# *Dhambi Isiyosameheka*

. . .?. . .Tunaimba nyimbo hizo, nazo zinaangaza nyuso zetu; kufikiria baada ya miaka elfu kumi hatutakuwa tumepungukiwa na wakati. Lakini mnajua, sasa ndio wakati tulio nao wa kumfanyia Bwana kazi, sivyo? Wakati pekee tulio nao ni katika kipindi hiki kidogo cha maisha ya kibinadamu, wakati tukiwa hapa. Nami ninaamini ya kwamba inatupasa kuweka kila dakika tunayoweza katika utumishi wa Bwana, tukifanya jambo fulani. Haidhuru ni nini, kama ni kuimba, kushuhudia, kufanya jambo fulani kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kwa maana wazieni tu, tutaimba tu miaka elfu kumi baada ya kufika huko. Hiyo ni ibada ya nyimbo tu, ni ninii tu, haipiti hiyo kabisa, mwajua, miaka elfu kumi. Kwa hiyo huo utakuwa wakati mzuri sana.

Sasa tunatangaza usiku wa leo, ninii tu. . .Sina budi kuondoka asubuhi kuelekea Idaho. Niwe nimeondoka siku chache, nirudi. Halafu Mungu akipenda, tunataka kuanzisha uamsho wa mtindo wa kale, papa hapa maskanini. Majuma machache yajayo, tutajua yote kuuhusu, Bwana akipenda. Na ni uamsho mzuri wa mafundisho, ninii tu. . .Tulitumbukiza mikono yetu kwenye mtungi wa asali asubuhi ya leo na tukawa na wakati mzuri, wa ajabu. Pia mnajua, kwenu nyote ambao hamkuwa hapa, hakika mlikosa ratiba ndefu. Hiyo ni ratiba ndefu, saa mbili, nilikuwa hapa nikifundisha. Na kisha nikajisikia vizuri sana, nimerudi tu hivi punde kutoka Colorado, nami najisikia vizuri sana, na kwa hiyo ni—nilikuwa nianzishe huo uamsho mara moja.

Na baadhi ya marafiki zangu wapendwa, ambao kamwe usingeweza kuwakatalia, Ndugu Arganbright, na wengi wao kutoka California, Wafanya Biashara Wakristo, waliniomba nikutane nao Idaho. Nami sina budi kwenda California asubuhi; niende mpaka Idaho, kwa ajili ya Jumanne. Nao wanashuka kwenda Snake River, na kadhalika, walitaka niende pamoja nao. Kwa hivyo sikuwa na mikutano iliyopangwa, kwa hivyo mimi . . . Mnajua, mtu akikutendea mema, unawapenda. Hiyo ni kweli. Wamekuwa wema kwangu. Kwa hiyo nikaingia na kumwomba Bwana, na ilionekana kana kwamba Yeye aliniambia ingekuwa ni sawa kwangu kwenda, kwa hiyo ninaenda basi.

2 Kisha nirudi, Mungu akipenda, na kuanzisha huo uamsho, na kuwa na wakati mzuri wa mtindo wa kale. Sasa tunataka mwe mkiutafakari, na kuuombea, kwamba Mungu atafungua tu madirisha ya Mbinguni na kutumwagia Roho wa uamsho juu yetu.

3 Kama tulivyosema asubuhi ya leo, mnajua, maji na. . .Kwa

mfano, mto, ningeweza kusema. Sasa, wakati ninii . . . Na wakati mwingine mto huo ni mkali sana, na unaruka-ruka na kutibuka, bali hauna maji zaidi ndani yake kuliko uliyo nayo unapokuwa mtulivu tu uwezavyo kuwa. Lakini una uamsho unaoendelea, mnaona, nao upepo unauvumia, na kuufanya urukeruke na kushangilia. Na jambo zuri kuhusu hilo, hufanya vijiti vyote na takataka zote zielee, kama nilivyosema, hata ufukoni.

4 Hivyo ndivyo uamsho unavyofanya, unaturusharusha tu huku na huku namna hiyo mpaka unatufikisha . . . Tunarukaruka tu *hapa* chini, na kurushwarushwa juu, na kurushwarushwa *huko*, na kupanda tukamwombee *huyu*, kisha tunashuka kwa jirani, mnaona. Muda si muda mwajua, Bwana anatufunulia, "Unajua, hukupaswa kumsengenya jirani huyo, kwa vyovyote vile."

"Naam, nitaenda nikamwambie aende kanisani."

5 Kidogo huo hurusha na kutoa takataka kidogo, mwajua. Hivyo ndivyo tunavyotaka kufanya katika wakati huu unaokuja.

6 Sasa, sitaki kuchukua muda wenu mwingi kupita kiasi, kwa maana najua kesho ni—ni Jumatatu, na ni siku ya kazi. Basi wakati wa uamsho, Mungu akipenda, tunataka tu kama saa moja na nusu kamili, au saa mbili, usiku; ibada ya nyimbo, na kisha tuingie moja kwa moja kulifundisha Neno.

7 Nami nafikiri nyimbo ni nzuri sana, lakini unaweza kuuharibu mkutano kwa nyimbo, unaona, nyingi mno. Mnaona? Tunaweza kuimba, lakini kile Nyumba ya Mungu ilicho, ni ya marekebisho, ni kwa ajili ya Neno, ya ufahamu, maagizo, tupate kujua jinsi ya kuenenda. Nami nafikiri mmeziandaa nyimbo zenu vizuri sasa, kana kwamba tu ilikuwa usiku wa leo. Hilo ni zuri sana.

8 Sasa, mnamo wakati huu, tutakuwa na nyimbo maalum, bila shaka. Hatuwezi kuzilundikia zote usiku mmoja, lakini, usiku baada ya usiku, tutakuwa na nyimbo maalum.

9 Nasi tunataka kuwaalika watu waingie, na, bila shaka huenda ikabidi kulitangaza mara moja tu, tutakaporudi. Nanyi muutarajie. Nasi tutaweka tangazo dogo gazetini, na—nanyi nyote mjitokeze. Sasa, hautakuwa ibada ya uponyaji. Utakuwa ni uamsho.

10 Sasa, uamsho haumaanishi kuwaleta waongofu wapya. Uamsho unamaanisha kuwaamsha walio waongofu tayari. Mnaona? Ni, *uamsho*, maana yake ni "kuamsha," mnaona, "kuinua," "kufanya hai tena." Nalo kanisa, wakati mwingine, tunalegea kidogo, na kwa hiyo tunatazamia mojawapo ya nyakati hizo za kale, kama tulivyozoea kuwa nazo, muda mrefu uliopita.

11 Gertie alinipigia simu muda mfupi uliopita, naye akasema yeye na Dada Angie wangekuja na kuniimbia ule *Wakati wa*

*Mkutano Wa Kambi* (miaka arobaini iliyopita). Kwa hivyo tunatarajia. . .Basi—basi muwaambie ndugu na dada wengine wa kanisa kwamba wote wamealikwa.

12 Sasa, usiku wa leo tunasoma somo lenye kina sana, lililotangazwa asubuhi ya leo. Nami bila shaka ninathamini ukarimu na fadhili za Ndugu yetu Neville. Sikuzote yu tayari kuketi nyuma na kuturuhusu sisi kwenda mbele na kadhalika. Huyo ni ndugu halisi. Anatoa mimbara yake moja kwa moja, kana kwamba si kitu, kwa hiyo, kufanya hivyo. Kwa hiyo, sisi, ninamthamini Ndugu Neville, sana. Na sikuzote amekuwa akijishirikisha katika kila jambo ambalo nimewahi kumwomba afanye. Ameshika tu kulifanya, namna hiyo tu, kwa hiyo ninathamini ndugu kama huyo.

13 Asubuhi hii. . .Tumekuwa tukisoma, kwa miezi minne iliyopita, ama kitu kama hicho, katika ule wa 9. . .au mlango wa 10 wa Kitabu cha Waebrania. Tulianzia kwenye kifungu cha 8, na tukaendelea hadi kwenye cha 25, nafikiri, asubuhi ya leo. Ndipo, usiku wa leo, nilitangaza kufundisha, Bwana akipenda, juu ya. . .*Dhambi Isiyosameheka*. Dhambi isiyosameheka ni gani?

14 Sasa, ili kupata msingi, tunataka kurudi katika kuyasoma Maandiko, na kurudia tamshi moja, ama mawili, ya asubuhi ya leo, halafu tuingie kwenye somo hili la kifungu cha 25, ama kifungu cha 26, hasa, na wa Kitabu cha Waebrania, mlango wa 10. Hebu tuanze kuvichambua kutoka kwenye kifungu cha 19 hivi, na tupate mambo machache.

15 Paulo, akizungumza hapa, akijaribu kutenganisha sheria na neema. Kanuni, au somo kuu, ni kutenganisha sheria na neema. Na hapa ndani analeta kule kumkaribia Kristo, kwa sheria; kumkaribia Mungu, kwa njia ya Kristo. Naye anayatenganisha, pamoja, akionyesha mahali kila sehemu inapotumika. Na zote, katika Injili, yote yanatumikia sehemu moja, ila tu ilikuwa katika vipindi mbalimbali vya wakati.

16 Halafu tumekuwa na mahali ambapo mwabudu alikuja, akatoa sadaka yake juu ya dhabihu inayotoka damu. Asubuhi ya leo tulifungua katika Ayubu, tukizungumza kiakili, tukamkuta Ayubu akiishi chini ya siku za dhabihu, na sadaka ya kuteketezwa. Naye akawazia labda kwa sababu watoto wake wanaweza kuwa wametenda dhambi kwa njia fulani, kwamba hawakuelewa kwamba walikuwa wametenda dhambi, Ayubu alitoa sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya watoto wake, apate kuwa na uhakika. Napenda hilo. Nanyi je? Kuwajali watoto wako! Kutoa sadaka ya kuteketezwa, kuomba chini ya dhabihu ya kifo cha kondoo, ili watoto wake wasipotee, ikiwa walikuwa wametenda dhambi, kwamba Mungu angewasamehe dhambi zao.

17 Ndipo tunaendelea kupitia Ayubu na kujua, mwishowe, jinsi jambo hilo lilivyoleta matokeo. Mungu, baada ya Ayubu kupitia wakati wake wa kurudiwa pamoja na majaribu. Mwishowe ilileta matokeo mema. Ayubu kamwe hakupoteza hata mmoja wa watoto wake. Alirudishiwa kondoo wake wote, ng'ombe wake wote, maksai wake wote, ngamia wake wote, maradufu. Kisha Mungu akamrejeshea, ama akampa watoto wake. Wote walikuwa wamekufa, kwa dunia; lakini walikuwa wakimngojea, Utukufuni, apate kuja. Hakuna hata mmoja wao aliyepotea, mnaona. Mungu alimpa Ayubu binti zake na wanawe. Kile inachomaanisha kuishi na kutembea katika Nuru ambayo unapaswa kutembelea, kuishia kanuni zote na vipindi vya wakati, wakati Yeye akitawala.

18 Tunaona katika Biblia, ya kwamba Zakaria, baba yake Yohana Mbatizaji, ambaye alikuwa binamu wa pili wa Yesu, ya kwamba alikuwa mtu mwenye haki. Je, mmeliona katika Maandiko? "Mtu mwenye haki, anayeishi chini ya sheria," na nyumbani mwake kulikuwa na maombi yaliyofanywa sikuzote. Naye Elisabeti, mkewe, alikuwa tasa. Na ilikuwa ni Roho Mtakatifu aliyemjia kwa mfano wa . . . ama, ilikuwa ni Gabrieli, malaika mkuu. Alipokuwa akitoa sadaka yake, ya kutikisa uvumba, kufukiza uvumba, maombi yalipokuwa yakifanywa hekaluni, ndipo malaika mkuu Gabrieli alipomjia, kwa maana alikuwa akitembea katika Nuru yote iliyombidi kutembelea.

19 Hayo tu ndiyo Mungu anayoweza kuyahitaji kwetu, Nuru yote tunayopaswa kutembelea.

20 Hapo ndipo Injili, le—lengo la kiakili la Injili, lilikuwa limeshindwa katika nchi ya kipagani, kwa sababu tumewaletea tu nadharia, ama theolojia fulani, hasa, ambayo mtu fulani ametunga. Na, katika hilo, tuliliwasilisha kwao, wala halina nguvu zaidi ya ibada zao wenyewe walizokuwa nazo.

21 Ikiwa, kwa maneno mengine, ikiwa wanafundishwa kwamba jua ni mamlaka kuu na linaitawala dunia. Linaitawala, kwa njia fulani, lakini, basi, wanaamini kwamba jua lina nguvu, kwamba kupitia jua mimea hutokea, kupitia kwa jua uhai huja, kupitia kwa jua huja . . . Vema, hiyo ni kweli kabisa, lakini jua ni uumbaji tu wa Muumba.

22 Tulikuwa na mmoja jukwaani kule. Sasa labda mmepata barua zake, wengi wenu mnaowajua wamishenari na kadhalika mle. Mmoja alijitokeza . . . Wao huketi chini na kuliangalia jua mpaka wanapofuka kabisa. Nao wanajisikia, kama jua litayazimisha macho yao, basi hawawezi kuona dhambi na mambo ya ulimwengu, wao ni vipofu kwa ulimwengu, na, basi, katika kufanya hivyo, mbona, "wataokolewa." Sasa, hayo ndiyo maarifa yote waliyo nayo juu ya Mungu. Wamefundishwa hayo, hata wanaamini ya kwamba hivyo ndivyo wanavyopaswa

kufanya, kutoa dhabihu, wakipofushwa macho yao na jua, “wataokolewa.”

23 Wengine hutembea motoni; wanajilaza juu ya misumari; wanainua mikono yao juu, wanasema kamwe hawataiweka chini mikono yao mpaka wapate amani. Nayo makucha yao ya vidole hukua kupitia sehemu ya nyuma ya mikono yao, namna *hiyo*, kwa miaka na miaka na miaka, na makucha ya mikono yanakua sana. Pasipo kuitenganisha mikono yao; wanaiinua juu, wakitembea namna hiyo. Waaminifu, waaminifu kabisa, bali hawana Injili.

24 Sasa, na, huo, ni wajibu wetu kuona ya kwamba wanadamu hao, kama tu tulivyo sisi. . . Na, hata hivyo, wao ni ndugu zetu, tukinena kimwili, kwa maana Mungu kwa damu moja aliumba watu wote. Kila mtu, kila mwanadamu, walitoka kwenye mti mmoja, Adamu, hapo mwanzo. Sasa, basi, kupitia hilo, ni wajibu wetu, kama ndugu Wakristo, kuwapelekea Injili ya kweli na iliyo hai. Ndipo, mle ndani, mtu atakapokuwa ni wa namna hii, mmoja anaabudu wanyama wadogo, na wadudu, na kadhalika. Basi, mnaona, wanaabudu kiumbe badala ya Muu-. . . Muumba. Ndipo wanapoisikia Injili ya Bwana Yesu mara moja. . . Wameisikia mara nyingi, kupitia maisha ya umishenari, kusambaza vitini, na kadhalika. Wanasema. . .

25 Nikasema, “Ni wangapi wenu enyi waungwana wanaojua habari za Bwana Yesu?” Kila mmoja wao. “Ni wangapi wenu wanaamini ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu?” Hakuna hata mmoja wao, mnaona. “Vema, mnafikiri alikuwa ni nini?”

“Loo, alikuwa mwalimu, kama tu wetu alivyokuwa,” na kadhalika. Mnaona?

26 Kwa sababu, hii, kwamba hakuna chochote, kupitia kwa yeyote wa miungu yao, ambacho kitaleta matokeo yoyote ya asili. Lakini kupitia Injili ya Bwana Yesu Kristo litatimia kila Neno alilosema. Na hiyo ni kweli. Hiyo inaleta tofauti.

27 Wakati maskini mtu huyu aliyesimama pale, kipofu, alikuwa hajaona kwa miaka na miaka. Nilisema, “Dini yenu inaweza kumfanyia nini mtu huyu?” Hakuna, bila shaka. Nikasema, “Lakini Yesu Kristo anaweza kuyafumbua macho yake sasa,” Naye akayafumbua. Kwa hiyo, huo—huo ndio ukweli wa Injili.

28 Sasa, Paulo hapa, akizungumza katika Waebrania, alikuwa akijaribu kuwaambia watu njia ya kumkaribia Mungu kupitia kwa Sadaka ya Bwana Yesu Kristo inayotoka damu. Hivyo ndivyo unavyomkaribia, ni kwa njia ya Yesu, kwa maana Yeye ndiye Mwana-Kondoo aondoaye dhambi ya ulimwengu. Naye Mungu alilitambua. Na sasa alisema. . .

29 Katika Agano la Kale, walipomleta mwana-kondoo, walitoa matoleo yao, dhabihu yao; wakamshika mwana-kondoo kwa

kichwa chake, huku akitetemeka na kufa; damu ikiruka juu ya maskini jamaa huyo, mshipa wake wa shingo ulipokatwa; ndipo wakatambua kwamba mwana-kondoo huyo alikuwa akifa badala yao. Ndipo, wakarudi nje, wakiwa na ukatili ule ule wa moyo kadiri walivyokuwa walipoingia. Tamaa ile ile ya kufanya uzinzi, tamaa ile ile ya kusema uongo, tamaa ile ile ya kuiba, na kuua, na kadhalika.

30 Lakini, mara mtu anapouweka mkono wake . . . Loo, jamani! Mtu akiweka mkono wake juu ya kichwa cha Yesu Kristo, na kuungama dhambi yake, akihisi maumivu na uchungu wa Kalvari, yale dhambi, yale Yeye aliyopaswa kulipa apate kumkomboa mtu kutoka dhambini! Naye Roho Mtakatifu, kutoka katika Damu ya Yesu Kristo, anakuja akimsafisha mtu huyo. Anatoka, kiumbe kipya, na ni mara moja tu. Anatoka akiwa mtu tofauti. Anatoka huku shida yote ya dhambi imetatuliwa milele. "Kwa maana kwa dhabihu moja," yasema Maandiko hapa, "amewakamilisha milele wale wanaotakaswa." Naye akasema, "Roho Mtakatifu anashuhudia vivyo hivyo." Mnaona?

31 "Hiyo dhabihu moja, milele, Yeye alitoa dhabihu Yake, akitoa uhai Wake Mwenyewe, akaketi mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu. Nasi tunaye Kuhani Mkuu anayeketi katika Ukuu wa Mungu, Uweponi mwa Muumba mkuu, akituombea juu ya maungamo yetu."

32 Kisha akasema hapa, katika kifungu cha 19:

> *Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu,*

33 Wazieni hilo, hakuna hofu! Hilo ndilo pigo kuu lililoko katika kanisa la Kikristo siku hizi, ni, "hofu." Na sababu ya wao kuhofu ni kwa sababu hawajafundishwa vyema, na kukalishwa vyema, juu ya Injili.

34 Hakuna sababu hata kidogo kwa nini mahali hapa padogo pasingeweza kuwa mzinga wa nyuki wa Nguvu za Mungu, ukivuma kwa Utukufu wa Mungu, wakiruka kutoka kila mahali. Maskini shimo hili dogo ukutani hapa, karibu hivyo, linajulikana ulimwenguni kote, mahali hapa padogo mnapoketi usiku wa leo; si kwa sababu ya William Branham, bali kwa sababu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, na Injili ambayo wameishindania. La, bwana, sikuwa na uhusiano wowote nayo, hata kidogo. Yeye Ndiye aliyefanya jambo hilo, na kufanya mahali hapa pajulikane ulimwenguni kote, wakati hapakuwa kitu ila jengo la dola elfu moja mia tano, ama kitu kama hicho, lililojengwa hapa juu, bila sakafu ndani yake. Lakini Mungu Mwenyezi ndiye anayefanya mambo hayo. Sasa ameninii . . .

> . . . tunao *ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu,*

*Kwa njia ile mpya na iliyo ya kweli, . . .*

35 Sio njia ya kale. "Kwa njia mpya na iliyo hai." Hiyo ilikuwa njia iliyokufa, utaratibu wa sheria; lakini sasa tunaingia kwa neema, kwa njia ya Roho Mtakatifu. Loo, natumaini mnaliona. Hakuna ambacho ungeweza kufanya. Sheria ilikuwa ni matendo, "msiguse, msishike, msionje, msile nyama, zishikeni sabato, miandamo ya mwezi," aina zote za ibada, kile ambacho mwanadamu alifanya. Lakini katika hii "njia mpya na iliyo hai," si kitu ambacho tungeweza kufanya. Ni kile anachotufanyia Yeye, kwa neema. Tunakikubali tu. Kristo huondoa dhambi. Tunaamini Hilo. Isikieni Injili, iaminini, ikubalini. Na basi kama kweli tukiikubali, kutoka kwenye vilindi vya moyo wetu, Mungu hutupa Roho Mtakatifu, kama shahidi.

36 Ndipo Roho Mtakatifu anakushuhudia kwamba dhambi zako zimekwisha, na umekufa kwa ulimwengu. Unainuka katika upya wa maisha, kutembea maisha mapya, kuishi maisha mapya, kuishi katika Nguvu na Uwepo wa Mungu. Sio kuchukuliwa na kila kitu tena, bali kuenenda kwa Roho, kama wana na binti za Mungu. Warumi 8:1, ilisema, "Sasa hakuna tena hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho."

37 Sasa, kwa wengi wenu sana ninyi watu hapa, wageni kutoka makanisa mengine, sitaki mfikiri kwamba mimi ni mpingaji makanisa mengine, na ninajaribu kulipapasa kanisa hili. Ninachojaribu kufanya ni kuondoa mambo ya kimwili katika kanisa hili. Na hilo ndilo jambo kuu. Nina mengi ya kufanya. Lakini, kujaribu ku—kufanya hivyo, kuifagia milango yetu wenyewe hapa. Lakini katika kufanya hivyo, inatupasa kutumia mifano mingine. Nanyi mnajua, ndugu, kutoka kanisani mwenu, sote tunahitaji kufagiliwa, kote. Mnaelewa hilo.

38 Kwa hiyo, jambo lake ni, ni kuona ya kwamba Mungu hatambui dhehebu lolote ama kundi lolote la watu. Kama wewe ni Mmethodisti, Yeye hakutambui kwa sababu wewe ni Mmethodisti. Kama wewe ni Mpentekoste, Yeye hakutambui kwa sababu wewe ni Mpentekoste. Anamtambua mtu binafsi tu, amina, ambaye amezaliwa, akazaliwa upya na Roho Mtakatifu, na kufanywa kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

39 Hayatambui madhehebu. Hayatambui makusanyiko makubwa. Mungu haji kamwe katika makusanyiko makubwa ati kwa sababu ni makusanyiko makubwa. Anakuja kwa sababu mioyo iko katika nia moja na inamtarajia aje. Mwangalie Yesu, kwa walio wanyenyekevu kabisa wa kanisa, "wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu."

40 Sasa, nilisema asubuhi ya leo, nami nitalisema tena sasa hivi, kwamba kanisa le—letu dogo hapa, kadiri tujuavyo, tunajaribu kusimama kwenye Neno la Mungu lisiloghoshiwa. Lazima litoke *Hapa*.

41 Makanisa, wanapounda makanisa yao, mambo wanayofanya, wanazuia baraka za Mungu, kwa theolojia yao, hata Mungu hawezi kuingia na kuwabariki watu Wake. Wanalifanya kanisa lao rasmi sana, gumu sana na baridi sana, hata Roho Mtakatifu hawezi kuingia kanisani. Na ndipo ibilisi alipoona alikuwa amefaulu, na wengine walikuwa wanaenda kupata ushindi kwa vyovyote vile, basi aliwaacha wafungue njia zingine ambazo hazikuwa ni za Injili, na kuwaingiza mbio kwenye ulokole. Hiyo ni kweli. Mnaona? Ama wanakuwa kundi la walokole, au kundi la waliojaa ubaridi. Lakini katikati ya barabara, ndipo pana Injili ya Bwana Yesu Kristo.

42 Kama nilivyonena asubuhi ya leo, na kuunga mkono hili sasa kwa swali hili kuu ninalojiandaa kuuliza katika muda mfupi, ni hili, kwamba mtu huchukua roho ya mtu mwingine. Jihadhari usije ukapata roho ya mtu fulani badala ya Roho wa Bwana. Ingia kanisa fulani, uangalie jinsi mchungaji anavyotenda, nawe utaona jinsi watu wanavyotenda. Unaona? Ikiwa mchungaji ni baridi sana na mgumu kweli kweli, hao watu watakuwa vivyo hivyo. Ukiingia mahali ambapo ni vurugu na ulokole, watu watakuwa vivyo hivyo.

43 Kwa hiyo, ndugu, tunapaswa kushukuru hapa, kwenye maskani usiku wa leo, kwa ajili ya mchungaji aliye na akili timamu, mwenye busara, na anahubiri Injili rahisi, kamili, huru, na katika nguvu Zake. Naam, bwana.

44 Kama kuna kitu ninachotaka kuwakilisha vema, katika ulimwengu huu, endapo sitauwakilisha ubinadamu vema, ninataka kumwakilisha Yesu Kristo katika Uzima Wake.

45 Nataka kuwa Mkristo wa Biblia. Yale Biblia isemayo, hayo ndiyo ninayotaka kuamini. Haijalishi ni nani anayepinga, au ni nani hapingi, sigombani nao, bali ninataka kuamini Biblia. *Hili* ni Neno la Mungu. Ninaamini kwamba Huo kweli ndio mpango wa wokovu. Neno la Mungu ndilo Mwamba pekee utakaosimama na kuzistahimili nyakati, ni Neno la Mungu. Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Kwa hiyo naamini *Hii* ndiyo Kweli. Hivi Mungu. . .

46 Ninalisema kwa unyenyekevu mbele ya maskini kanisa langu hivi. Nisingeweza kulisema hilo katika mikutano mikubwa, kwa maana wangelishambulia, na kadhalika. Lakini, kama mwonaji ambaye Mungu huonyesha maono, hilo halinifanyi mimi kuwa zaidi ya yule mlevi aliyeongoka dakika kumi zilizopita, mahali fulani. Hiyo ni kweli. Yeye ni Mkristo, kadiri nilivyo mimi, ataenda Mbingu ile ile, akazifurahie baraka zile zile na mambo ambayo ningefurahia, ama mtu mwingine yeyote.

47 Hakuna watu mashuhuri na watu wakubwa katika Ufalme wa Mungu. Sisi sote ni mmoja. Hiyo ni kweli. Kila mtu ni mtu yule yule, ndugu na dada. Iwe sisi ni wa manjano, weusi, weupe, chochote tulicho, sisi ni mmoja katika Kristo Yesu. Hakuna DD,

L maradufu, na jamaa mdogo, mashemasi na mabawabu, ama chochote walicho. Wote ni sawa katika Kristo Yesu, Mtu mmoja. Sisi sio mmoja juu ya mwingine. Ndiyo maana sisi ni ndugu na dada katika Bwana Yesu Kristo.

48 Na basi tunapokutana pamoja, tukiketi katika mahali pa Mbinguni, kwa nia moja, moyo mmoja katika nia moja, basi Roho Mtakatifu anaweza kuingia na kutubariki, na kutupa Neno la thamani la Mungu. Kisha, katika jambo hili, mara nyingi, kupitia maono, huona mambo.

49 Jambo la kwanza wakati mtu anaponiambia, au ninasikia kwenye kanda, kwamba nimeona ono na kutabiri jambo fulani; kabla sijasema lolote kuhusu hilo ono, jambo lolote, kwanza ninalichunguza hilo ono kwa Neno la Mungu. Na kama si kulingana na Neno la Mungu, ningesema ningesema ni. . . Umbali huu, Mungu ashukuriwe, daima imekuwa ni kulingana na Neno. Lakini kama kamwe ingekuwa kinyume na Neno la Mungu, ningesema, "Msilisikilize, kwa sababu ni la uwongo." *Hili* ndilo Kweli, papa hapa, Neno la Mungu.

50 Ndipo, tukija kwa busara, akili timamu, kwa Mungu, tunapokuja bila uovu wowote, chuki yoyote; kwa moyo wazi, tayari kujifunza, Mungu anaweza kufundisha. Wakati tuko tayari kujifunza! Lakini hatuna budi kwanza kuweka kando mapokeo, tuweke kando mawazo ambayo tumefundishwa. Sasa, najua mama alikufundisha mambo ambayo yalikuwa mazuri sana, na kadhalika, lakini wakati mwingine mama alikosea mambo.

51 Nina mama anayeketi papa hapa, ambaye mimi. . .somo lenyewe ninaloendea baada ya dakika chache, aliniambia, miaka kadhaa iliyopita, kwamba alifikiri "dhambi isiyosameheka ilikuwa ni kwa mwa—mwanamke kuninii. . .kisa cha kutoa mimba." Kwa maneno mengine, kuutoa uhai wa mtoto, kabla hajazaliwa. Kasema, "Angewezaje kamwe kusamehewa hilo?" Mama, kadiri alivyojua, kwa yote aliyojua, hiyo ilikuwa ni kweli. Mnaona? Lakini si kweli kulingana na Neno la Mungu, kwa hiyo hiyo inaleta tofauti.

52 Kwa hiyo mtu fulani akasema, "Nilizaliwa Mkatoliki. Mama alikuwa Mkatoliki. Alinilea Mkatoliki. Nitabaki Mkatoliki."

53 Vema, nililelewa Mbaptisti, bali sikubaki Mbaptisti. Nilipoona Neno la Mungu likisemwa kinyume na yale fundisho la Kibaptisti lilivyokuwa, niliamini Neno la Mungu na kuacha neno la kila mtu mwingine liwe uongo. Hiyo ni. . .Sina ugomvi na huyo mtu. Nasema, "Ndugu, *Hili* ndilo ninaloamini. Bado ningali ndugu yako, lakini ninaamini *Hili* ndilo Neno la Mungu."

54 Sasa, na unapotulia, sawa kimsingi, ndipo unakuwa na ujasiri wa kuingia.

55 Sasa, najua watu, na nyote mnapaswa kukubali, kwamba tunao watu katika vikundi vya utakatifu, tunao watu katika makundi ya Kipentekoste, tunao watu katika ma—makundi ya Wanazarayo, na katika Pilgrim Holiness, na katika Methodisti, na Baptisti, na wote, wanaojifanya tu kuwa Wakristo, ambao si Wakristo. Ndani ya mioyo yao wanajua wao si Wakristo. Lakini siamini kuna mwanaume au mwanamke yeyote katika lolote la makundi hayo, angeweza kamwe kumkabili Yesu Kristo na kutubu dhambi zao kwa kweli, kwa moyo wa kweli, uliojisalimisha kikamilifu, akisema, "Bwana, kweli ninaamini," ila ambao Mungu angeweka juu yao ubatizo wa Roho Mtakatifu wakati huo hasa.

56 Sasa, wewe ni mwaminio, lakini Mungu haitambui imani yako mpaka atakapokuthibitishia. Amina. Loo, ndugu, hebu nikwambie jambo fulani. Wakati imani yako. . .Inaweza kutambuliwa katika mawazo yako mwenyewe, lakini inapoingia katika mawazo ya Mungu, Mungu huweka muhuri imani hiyo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ibrahimu alimwamini Mungu, naye akahesabiwa jambo hili kuwa haki, ndipo Mungu akampa muhuri wa tohara kama ishara kwamba alikuwa amemkubali. Haleluya! Na Muhuri wa Mungu aliye hai, siku hizi, (yachunguzeni Maandiko,) ni ubatizo wa Roho Mtakatifu juu ya moyo wa mwanadamu. Amina. Waefeso 4:30, ilisema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Muhuri wa Mungu, Mungu akikutambua wewe kama mwaminio, hukutia muhuri akakuweka katika Mwili kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

57 Basi ikiwa hujadanganywa, kuamini nadharia fulani, hisia fulani, kitu fulani kingine. . .ambacho ni sawa; sina neno dhidi yake. Vyovyote Mungu anavyokupa, hiyo ni kazi ya Mungu, na yako, unaona. Lakini wakati mtu anapozaliwa kwa Roho wa Mungu, utampata akiwa na ujasiri na ni mnyenyekevu tu awezavyo kuwa, anaenda kwenye Kiti cha neema na kujua kwamba ana haki ya kula kutoka kwenye Mti wa Uzima. Kwa maana, jambo fulani limetokea kwa mtu huyo, ambaye ana uzoefu wake, ambao hajawahi kuupata mahali pengine popote duniani. Na kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu ana ujuzi ndani yake mwenyewe, hata wanajua moja kwa moja, wakati lilipotukia, jinsi lilivyotukia, na lilikuwa na matokeo ya namna gani kwao. Kila mwanamume na mwanamke ambaye amewahi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, jambo fulani lilitokea, jambo fulani linabadilika tu. Ni. . .Ni nini? Ni uongofu.

58 Kama tulivyosema asubuhi ya leo; una kitambaa kikuukuu pale, kichafu tu kiwezavyo kuwa, kilichojaa wino na kadhalika. Hakuna kitu kinachoweza kuuondoa. Hebu kichovye hicho ndani ya mkebe uliojaa Kitoa madoa, au beseni, kitoe, ni

cheupe tu kiwezavyo kuwa. Hivyo ndivyo Damu ya Yesu Kristo inavyofanya kwa mwaminio anayeungama dhambi yake. Lilisema:

> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Wenye dhambi wanapotumbukizwa ndani ya
> hiyo gharika,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi.

59 Ndipo, Mungu anapotikisa hilo shuka na kuona kwamba limekaushwa na pepo takatifu za Mungu zinazokuja kama upepo wa nguvu ukienda kasi kutoka Mbinguni, Yeye anamchukua Roho Mtakatifu na kumtia huyo muhuri hata Siku ya Ukombozi namna hiyo.

60 Ndipo ibilisi anautazama Muhuri huo, hawezi kuukaribia. Anaweza kuutania, na kuuvumia, na kuugombanisha, lakini hawezi kuufikia. Hiyo ni kweli. Hawezi kuupata, kwa sababu kuna Muhuri wa Mungu unaomzuia, haleluya, unamzuia kuugusa. Hiyo ni mali ya Mungu binafsi. Haleluya! Naam, bwana.

61 Huo ndio unaomfanya mtu kutembea kwa ujasiri. Hawaogopi kurudi nyuma. La, bwana. Hawaogopi kile ibilisi asemacho.

62 Kuna jambo moja kulihusu, unaweza kwenda kurejelea sababu zako, na unaweza kujifunga kwenye hoja. Usijaribu kulihoji. Unasema, "Sasa hebu nione. Labda ningefanya *hivi*." Usilihoji. Liamini. Mungu haji kwa hoja. Yote, yote hayana busara; hakuna mtu anayeweza kumwelewa Mungu. Hujawahi kumwelewa, nao hawatawahi. Humjui Mungu kwa hoja.

63 Unamjua Mungu kwa imani rahisi ya kitoto, kulikubali Neno Lake. Unasema ni Kweli, na kuliamini. Hivyo ndivyo unavyomjua Mungu, ni kwa imani; si kwa hoja, uwezo wako wa kuhoji ndani yako. Lakini imani hutoka kwa Mungu. Imani ni kitu ambacho kimezaliwa ndani yako, kitu ambacho Mungu anakupa. "Na ni hakika ya mambo yatarajiwayo, na bayana ya mambo yasiyohojiwa." Haleluya!

64 Hapo ndipo inapotoka, kupitia hapo, kupitia kwa nguvu zisizoghoshiwa za Bwana Yesu Kristo, zinazokifanya kiumbe kuwa mtu mpya, zinambatiza upya katika Roho Mtakatifu. Zinamwosha, kumwinua juu, na kumtia muhuri katika Ufalme wa Mungu, ndipo anasimama, akijua mahali alipo. Mashetani wote kuzimuni wasingeweza kumtikisa kutoka humo. Unaweza kumwelekezea bombomu . . .

65 Tayari imejaribiwa. Majuma machache yaliyopita, niliingia kwenye mapango ya kuzikia ambamo mifupa ya kale na mafuvu ya vichwa, karibu kiasi *hicho* tu chao ndicho kimesalia, ambapo watakatifu na wafia imani walikufa. Nilisimama kwenye ule

uwanja ambapo waliwalisha kwa simba, na kadhalika. Na bila kupepesa jicho, wakafa; wakijua jambo hili, kwamba "wanamjua katika Nguvu za kufufuka Kwake," kwamba siku moja, wakitetemeka, kutoka hapo watatokea, watakatifu wa Mungu aliye hai waliooshwa kwa Damu. Loo, ndugu, mtu ambaye amewahi kuwasiliana na Mungu hawezi kuwa vile vile tena.

66 Ninakumbuka wakati maskini jeshi, maskini jamaa yule alipotokea kule kukutana na Yesu Kristo, akiwa amerukwa na akili. Nao pepo walikuwa wamempagaa mpaka akawa jeshi. Lakini mara alipokuja Uweponi mwa Kristo, aliendа nyumbani kuwaambia watu wake mambo mema ambayo Mungu alikuwa amemtendea.

67 Wanasema kwamba dini inakutia wazimu. Haikutii wazimu. Huna akili timamu mpaka umpate Yesu Kristo, kwa maana Yeye ndiye Mwanzilishi pekee wa Uzima, ambaye anaweza kukupa akili yako timamu.

> . . . basi tuna *ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu* Kristo, (amina)
>
> *Kwa njia mpya iliyo hai tuliyofunguliwa, kupitia kwenye lile pazia, yaani, mwili wake;*

68 Mwili hufanya nini? Mwili huifunika tu damu. Damu ndiyo uhai. Hiyo ndiyo njia pekee inayodumisha uhai mwilini mwangu, ni kwa ngozi na nyama na tishu na mishipa, na kadhalika, kuishikilia damu mahali pake, ili ipate kuipa uhai maskani hii ninamoishi. Hiyo ni kweli?

69 Hiyo ndiyo iliyomficha Mungu kutoka kwa wanadamu, ilikuwa ni Damu na mishipa na ngozi za Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kuzaliwa Kwake kusikoghoshiwa, Ambaye Mungu Baba alimtia uvuli bikira Mariamu na kuumba ndani yake chembechembe ya Damu ya Nafsi Yake Mwenyewe, uumbaji. Na, humo ndani, ngozi Yake ilizuia asionekane na mwanadamu.

70 Lakini siku moja dhambi ya mwanadamu iliufungua moyo Wake, kwa mkuki, na Damu Yake ikaanguka ardhini. Ilitolewa bure kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Na imefunuliwa leo. Na wakati Damu hiyo ilipotoka, pia Roho alitoka. Na kwa kuoshwa kwa maji kwa Damu, kupitia kwa Roho, tunazaliwa katika Ufalme wa Mungu, viumbe vipya katika Kristo Yesu.

71 Naye Mungu akauchukua mwili huo uliokufa, ungali umelala kaburini, na kuufufua kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, ameketi mkono wa kuume wa ukuu Wake, usiku wa leo, akifanya maombezi. Tunapaswa kuwa watu wa aina gani, waoga, tukighairi, ukiogopa kumwambia bosi kwamba umeokoka, au umezaliwa mara ya pili, unaogopa kumtolea mlevi ushuhuda? "Tuna ujasiri," haleluya, "wa kuingia Patakatifu sana kwa Damu ya Yesu Kristo."

72 Lo, itaita. . .Watakuita mtakatifu anayejibingirisha. Watakuita kila kitu. Ni tofauti gani hiyo? Walimwita "Beelzebuli." Mnaona? Lakini, inaleta tofauti gani, wanachokuita? Ni kile ambacho Mungu anakuita. Ulimwengu ulisema, "Mtakatifu anayejibingirisha! Asiye na elimu! Ulokole!" Kanisa lilisema, "Ameenda kombo. Yeye, amerukwa na akili."

73 Lakini Mungu alisema, "Huyu ni Mwanangu." Afadhali niwe na hilo kuliko sifa zote za mwanadamu. Sitaki mtu kunipigapiga mgongoni. Nataka Kristo anishike mkono. Amina. Je, huo ndio ushuhuda wako?

74 Inanikumbusha juu ya maskini Daudi wa kale, wakati mmoja, wakati sanduku lilipokuwa huko chini miongoni mwa Wafilisti, na kadhalika. Uamsho ulikuwa haupo, wa Israeli. Naye Daudi alikuwa amesimama, siku moja, naye akatazama ng'ambo ya kilima akaona lile sanduku likija. Akawa mtakatifu anayejibingirisha. Akaanza kucheza na kukimbia huku na huko, kwa nguvu tu alivyoweza. Ndipo mke wake mtarajiwa akamdhihaki. "Mbona," akasema, "ati hupendi hilo? Huh? Tazama hili!" Naye huyo akashuka chini, ndipo akazunguka na kuzunguka, akicheza, kwa nguvu tu alivyoweza.

75 Mkewe aliletewa fedheha. Alifanywa tasa. Wala hakuwahi kuzaa watoto. Nalo jina lake likafa katika Israeli.

76 Lakini hili hapa lililotokea. Mungu aliangalia chini kutoka Mbinguni, na kusema, "Daudi, wewe ni mtu aupendezaye moyo Wangu." Naam, bwana.

77 Ni afadhali niwe na hilo kuliko umaarufu wote wa wanawake, wanaume, ama yeyote yule katika dunia hii. Afadhali nipate kibali kwa Mungu; Mungu anasema, "Ninaye mtumishi ninayeweza kuweka kidole Changu juu yake, naye ataniamini na kunitumaini." Hiyo ni kweli.

78 Huwezi kulifanya kwa maungamo nusu-nusu. Huwezi kulifanya kwa akili iliyofumwa. Huna budi kulifanya kwa imani safi isiyoghoshiwa kwa Damu ya Yesu Kristo. Umeingia Huko juu na unajua umemgusa Mungu kwa mkono, nawe ni mtumishi Wake. Huogopi chochote basi. "Tumepaingia kwa njia mpya na iliyo hai, kupitia Damu hii, kupitia pazia Lake lililoifunika." Mbele kidogo tu. Kuwa na. . .

> *Tena tunaye kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu,* yaani, Kristo; (sikilizeni hapa)
>
> *Na tukaribie kwa moyo wa kweli,* na kwa dhamiri ya. . .na *imani,* na dhamiri yetu imenyunyiziwa—imenyunyiziwa. . .kutoka kwa maovu, *na tumeoshwa miili kwa maji safi.*

79 Tumelipitia asubuhi ya leo. Sasa maji. . .*Kunyunyiziwa* hapo linamaanisha "kutikiswa na kuondolewa." Dhamiri

yetu, pamoja na shida ya dhambi, uovu na giza vilitikiswa vikaondolewa kwake. "Huku miili yetu imeoshwa kwa maji safi," kwa ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo.

80 Kumwendea Mungu kwa uhuru na kwa ujasiri, nikijua haya, kwamba, "Uovu nilioupenda wakati mmoja umepita, nikijua kwamba maisha niliyoishi wakati mmoja sasa yamekoma. Si kwa sababu nilifanya hivyo; kwa sababu Kitu fulani kiliingia ndani yangu na kulifanya Chenyewe. Kwa neema aliniokoa. Nilimwamini. Akanipa Roho Mtakatifu. Mambo ambayo wakati mmoja niliyachukia, sasa ninayapenda. Kujitolea, ilikuwa vigumu kwangu kwenda kanisani; ninapenda kwenda sasa. Kuwasikia watu wakiimba na kupaza sauti na kushuhudia, nilikuchukia; ninakupenda sasa. Kitu fulani kimenibadilisha. Basi, nina 'njia mpya na iliyo hai.' Kitu fulani kimetia nanga *hapa*. Ninajua nilipoingia majini, nao wakanibatiza kwa Jina la Bwana Yesu Kristo."

81 Yeye alisema, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

82 Nimebishaniwa, nikagombanishwa, nikanenwa mabaya, nikadhihakiwa, haileti tofauti hata kidogo. "Mungu alisema hivyo, nami ninaliamini! Na ni hivyo hasa." Nilisimama pale pale, vivyo hivyo tu, nikitikisa moja kwa moja.

Kasema, "Wewe ni Yesu Pekee. Wewe ni wa Umoja. Wewe ni *hili*."

83 Sijali wanachosema. Ninaamini Neno la Mungu kuwa ni Kweli. Wala sijui jinsi ilivyo maarufu, na hiyo haileti tofauti yoyote jinsi unavyokuwa maarufu hapa. Ni jinsi ulivyo maarufu Huko juu.

84 Mmoja wa watu mashuhuri hivi majuzi aliombwa kuhubiri hilo. Akasema, "Hiyo ni Kweli, lakini kama ningesema hiyo, kusanyiko langu lingeondoka."

85 Nikasema, "Afadhali nihubirie kuta nne, ile Kweli," Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto, "kuliko kupatana kwa Injili." Naam, bwana.

86 Kwa maana, siku moja Kitabu hiki kitanihukumu. Hiyo ni kweli. Maneno ya Mungu, Hapo, yatakuwa Hakimu wangu kwenye Siku ya Hukumu. Sina budi kuihubiri Kweli bila kujali jinsi inavyoumiza au kile inachoumiza.

87 Sikilizeni hapa sasa. Sasa tunaendelea.

> *Na tulishike sana ungamo* letu *la tumaini letu, lisigeuke; (. . .yeye aliyeahidi ni mwaminifu;)*
>
> *Tukaangaliane mmoja kwa mwingine na* kuhimizana *katika upendo na matendo mema:*

88 *Kuhimizana* hapo kunamaanisha "kutia moyo." Tuhimizane sisi kwa sisi kwa upendo na matendo mema. Ukimwona ndugu kanisani, aliye na neno dhidi ya ndugu mwenziwe, usiseme jambo la kuchochea kitu hicho, bali sema jambo ambalo litawaleta pamoja. "Tuhimizane katika matendo mema na katika upendo," ndivyo tunavyopaswa kufanya. Hiyo ni nini? Hiyo ni mtu ambaye amezaliwa mara ya pili.

89 Iwapo wewe, ndugu yangu, usiku wa leo, hujisikii hivyo unapowaona ndugu zako wakikosana, na maneno makali kati ya mtu na mwenziwe, ikiwa hujisikii kuwaleta pamoja, ni wakati wako wa kwenda madhabahuni. Hiyo ni kweli. Kuna kitu kimetokea maishani mwako. Kuna kitu umedanganyiwa. Huna ujuzi ambao Mungu anataka uwe nao.

90 Kwa maana, Yesu, alipotukanwa, hakutukana tena. Naye alinenewa maovu, hakujibu. Na wakati Yeye... Walipomfanyia maovu, Yeye aligeuka na kuwatendea mema. Walipomtesa na kumtundika msalabani, aliangalia chini na kusema, "Baba, wasamehe, kwa maana hawajui watendalo."

91 Kama Roho wa namna hiyo hayuko ndani yako, Roho Mtakatifu hajawahi kuingia ndani yako bado, kwa maana huyo alikuwa ndiye Roho yule yule aliyekuwa juu ya Kristo Yesu. Biblia ilisema, "Na awe ndani yenu." Kristo yuko ndani ya Kanisa Lake.

92 Sasa, Maskani ya Branham, ninyi kundi hapa, hatuna dhehebu lolote, hatuna kadi zo—zozote za kutia sahihi, ama kadhalika. Kitu pekee tulicho nacho hapa ni ushirika. Nanyi mnaoshiriki pamoja nasi katika Yesu Kristo usiku wa leo, na kufanya ushirika kila usiku na kila wakati, sikuzote tunafurahia kuwa pamoja nanyi hapa. Tunawatakeni muwe hapa. Sio lazima mjiunge nasi. Sisi... kitu pekee unachopaswa kufanya ni kuja kuabudu pamoja nasi. Na tunatarajia kila mmoja wenu kuishikilia siri ya kweli ya Mungu moyoni mwako, bila kuyumbayumba. Njoni kwenye ibada kisha mje madhabahuni, na kadhalika, na mpendane, na muwe na upatanifu ninyi kwa ninyi.

93 Na ukimwona ndugu akitoka kwenye njia, mwendee, upatanishwe naye ukiweza. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo tunalopaswa kufanya. Na, marafiki, iwapo kamwe... Unafanya nini, ikiwa hufanyi hivyo? Unajifanya tu kiumbe chenye mashaka, wala sio Mkristo, hiyo ni kweli, na yote unayofanya ni bure.

94 Hivi Yesu hakusema, "Mnaniabudu bure, mkifundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu?"

95 Unasema, "Vema, nilijiunga na kanisa. Niliweka jina langu kwenye kitabu. Nilifanya mambo haya." Hilo halina uhusiano wowote nalo.

96 "Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hataingia kamwe katika Ufalme."

97 Angalieni, tukija sasa kwenye kifungu cha mwisho, kabla tu ya kufunga, ama kabla ya kuingia katika somo langu kuu. Kisha tutaninii . . . Sitawaweka muda mrefu kupita kiasi.

> *Wala tusiache kukusanyika* . . . ninyi wenyewe *pamoja* (kuhudhuria kanisa), . . . *kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia*, zaidi.

98 Watu wakiacha kwenda kanisani. Makanisa yanaanza kuhamwa sasa. Vita vimekwisha. Kila mtu ameshiba, na ana nguo za kubadilisha, ana kazi nzuri sana, ametulia.

99 Hawana muda wa kukungojea unapoenda dukani. Nilipiga simu hivi majuzi, kutengenezewa jiko langu. Kasema, "Je, sisi ndio tulioliweka ndani?"

Kasema, "La, mtu mwingine, lakini walifunga biashara."

100 "Basi," kasema, "waone hao watu waliofunga biashara." Naam. Hawajali kabisa. Hivi majuzi, miaka michache iliyopita, wangeomba kila biashara waliyoweza. Lakini, wana pesa za kutosha. Hawajali; wanaachilia.

101 Lakini hebu niwaambieni, mambo hayo yatatoboa mashimo yaliyooza ndani yako. Lakini alisema:

> Usitamani utajiri wa ulimwengu huu usio na maana,
> Ambao huoza kwa upesi sana,
> Tafuta kupata hazina za Mbinguni,
> Hazitapita kamwe!

102 Nimepitia kwenye kuzorota kwa uchumi. Nimepitia mafanikio. Nimeyaona, kwa jumla. Lakini nisingeuachilia mkono wa Yesu Kristo, kwa ajili ya pesa zote na mali ambazo ungeweza kuzilundika juu ya uso wa dunia hii, na chochote kile. Yeye ni Rafiki yangu wakati nimefilisika. Yeye ni Rafiki yangu ninapokuwa na mengi. Ninampenda ninaposhikwa na njaa. Ninampenda ninaposhiba. Ninampenda ninapokuwa katika huzuni. Ninampenda wakati nikiwa na furaha. Ninampenda kwa sababu nampenda, kwa maana alinipenda kwanza. Amina. Haleluya!

103 Nilipokuwa mgonjwa, nimelala, nikifa, Yeye alikuwa Rafiki yangu. Ninapojisikia vizuri, usiku wa leo, mwenye furaha, Yeye angali ni Rafiki yangu. Nitakapolala kule, nikifa, mahali fulani, na mishipa yangu baridi ikipanda mikononi mwangu namna hiyo, Yeye atakuwa Rafiki yangu wakati huo. Na wakati nyuzi hizi nyepesi ambazo ninatembea—ninatembelea, zikivunjika, nami nizame katika Umilele, Yeye atakuwa Rafiki yangu wakati huo. Wakati nyakati zinapopita, baada ya miaka elfu kumi, mmeimba nyimbo zenu za yubile, Yeye angali atakuwa Rafiki yangu wakati huo. Naam, bwana. Wakati hakutakuwako na

mwezi tena, hakuna jua tena, hakuna dunia tena, Yeye bado atakuwa ni Rafiki yangu wakati huo, kadiri nyakati zinavyopita. Loo, jinsi tunavyopaswa kumpenda!

104 Kazi yako ni nini? Ni nini chochote ulicho nacho? Umaarufu wako ni nini? Ninii yako. . .U nani wewe, kwa vyovyote vile? Hiyo ni kweli. Wewe ni nani kumpa Mungu kisogo? Wewe ni nani kukataa, kutotii Neno moja ambalo Yeye angelisema? Wewe ni nani hata kuligeuzia Neno la Mungu kichwa chako, kwa sababu mhubiri fulani ama mtu mwingine alikwambia ya kwamba lilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine? Wewe ni nani hata kumwamini mwanadamu badala ya Mungu? Wewe mwamini Mungu badala ya mwanadamu. Hiyo ndiyo njia ya kuwa marafiki na Mungu.

105 Sasa angalieni. Akiona haya yote pamoja, ndipo Paulo anatoa kilele hiki kikuu, jibu hili kuu sasa. Hili hapa linakuja. Angalieni.

> *Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya. . . kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya* dhambi,

> *Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya. . . kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya* dhambi,

106 Hebu na tulichambue, kwa dakika moja tu, hapa katika kufunga. Nitawaachieni ninyi. Na papa hapa ndipo ninapoweka msingi wa uamsho wangu, unaokuja, moja kwa moja kwenye Maandiko haya.

> *. . .kama tukifanya dhambi kusudi baada ya. . . kuupokea ujuzi wa. . .kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya* dhambi, (angalieni)

> *Bali kuna ku—kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kumla* yeye apingaye.

> *Mtu aliyeidharau sheria ya Musa alikufa* chini ya. . . *alikufa pasipo huruma, kwa* ninii. . .*kwa neno la mashahidi wawili au watatu:*

> *Hivi haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi,* naam. . . mtu aliyeikanyaga *damu ya* Yesu Kristo ya *agano*, mliyotakaswa kwayo, *kuwa ni kitu ovyo,. . .kuyafanyia jeuri* matendo *ya neema?*

107 Itakuwa adhabu kubwa zaidi jinsi gani! Wakati chini ya mwana-kondoo anayekufa, ambapo mtu aliyeidharau au kuikataa, kwa sheria ya Musa, ilibidi afe pasipo huruma, kwa sababu mwana-kondoo alikuwa amekufa badala yake. Ni zaidi sana vipi mtu, aliyeikataa, ambaye anadharau Damu ya Yesu Kristo!

108 Sasa, jambo la kwanza tunalotaka kujua, dhambi isiyosameheka ni ipi? Baadhi yao walisema, “Ni kujiua.”

Baadhi yao walisema, “Ni—ni mama anayemtupa mtoto wake,” kisa cha kutoa mimba. Wengine wamesema *hivi*. Wengine wame—wamesema, “Kwa sababu wakati mmoja ulikuwa na Roho Mtakatifu, kisha ukamwasi Roho Mtakatifu, hiyo ndiyo dhambi isiyosameheka.” Siyo. La, bwana.

109 Hebu tuliangalie, kwa akili. Hebu tuliangalie, Neno la Mungu. Sasa, katika Kitabu cha—cha Mathayo, mlango wa 12, Yesu alikuwa amemtoa pepo bubu na kipofu, ama pepo bubu na kiziwi, naamini ndivyo ilivyokuwa, kutoka kwa mtu. Basi alipoitoa, kiziwi na bubu akanena. Watu wakageuka, wakamwangalia; wakasema, “Mbona, Yeye hutoa pepo kwa Beelzebuli, mkuu wa pepo.” Ndipo Yesu akageuka na kuwauliza . . .

110 Wangewezaje kuamini, huku mioyo yao imejaa uovu na jinsi walivyokuwa? Kwa nini, kwa nini akawahukumu? Kwa nini? Kwa sababu, hii, kwamba Neno la Mungu Lenyewe liliwahukumu. Kwa kuwa, Yesu . . .

111 Je, Petro hakusema, katika Siku ya Pentekoste, kwenye Matendo 2, yapata kifungu cha 24, 23 na 24? Alisema, “Enyi watu wa Israeli! Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu; Mungu alimthibitisha kwa ishara na maajabu na miujiza aliyofanya mbele yenu, ambayo ninyi pia ni mashahidi.”

112 Hapa, jambo la kwanza tunalopaswa kuwazia sasa, wakati sisi . . . Naye Yesu aliwaambia hao Mafarisayo, katika mlango wa 12 pale. Alisema:

> . . . kama mtu akisema neno *dhidi ya Mwana wa Adamu, atasamehewa: lakini* mtu yeyote atakayesema *neno dhidi ya Roho Mtakatifu,* kamwe *hatasamehewa, . . . katika ulimwengu huu, wala . . . ulimwengu ujao.*

113 Ni nini “Kunena mabaya dhidi ya,” “kunena dhidi ya Roho Mtakatifu,” “kunena dhidi ya”?

114 Sasa, unaweza kuwa umekosea, useme, “Utendaji kazi wa Roho Mtakatifu . . . Mtu akipaza sauti, inaweza kuwa ni Roho Mtakatifu.” Hiyo inaweza ikawa, na inaweza isiwe. Unasema, “Kunena kwa lugha, yeye akinena kwa lugha, je, ni Roho Mtakatifu anayenena kwake?” Hiyo inaweza iwe, na huenda isiwe. Hiyo ni kweli kabisa. Maana, nimeishi kuona wakati ambapo ninajua ya kwamba kila kitu kinachonena kwa lugha hakina Roho Mtakatifu juu yao.

115 Nimewaona pepo wakinena kwa lugha. Nimewaona waganga wakinena kwa lugha. Nimewaona wakinywa damu kutoka katika fuvu la kichwa cha binadamu, na kunena kwa lugha. Nimeona penseli zimewekwa juu ya meza, na kuandika katika lugha zisizojulikana, na wachawi wanaisoma. Hiyo haimaanishi kwamba wao ni Mkristo.

116 Nimewaona wakipaza sauti, na kuruka-ruka, na kumsifu Bwana; kisha wanatoka kwenda kuiba, na kusema uwongo, na kudanganya, na chochote kile. Najua hayo hayatoki kwa Mungu.

117 Lakini nawaambia, ndugu, palipo na upendo mkamilifu wa Kiungu wa Mungu ukitulia moyoni, uliotiwa muhuri, yeye yule jana, leo, ukiendelea mbele, unaweza kuanza kuwazia jambo hilo. Yesu alisema, "Hivyo watu wote watajua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mnapokuwa na upendo ninyi kwa ninyi."

118 "Palipo na lugha, zitakoma. Palipo na maarifa, yatatoweka. Palipo na imani, itashindwa," na mambo haya yote hapa. "Lakini ijapo ile iliyo kamili, ambayo ni upendo, hautapita kamwe," hiyo ni kweli, upendo wa Kristo.

119 Siwezi kuamua kwa chochote unachofanya. Mwamuzi pekee aliyepo ni Mwenyezi Mungu. Lakini Yesu alisema, "Kwa matunda yao mtawatambua."

120 Sasa, tunajua jambo moja. Sasa angalieni hapa. Hiki hapa kilele cha kila kifungu katika Biblia. Tutakichukua tu baada ya dakika chache na kuwaonyesha kwamba, ilinenwa kila mahali, juu ya dhambi isiyosameheka, isiyosamehewa. Ndipo Paulo anakuja hapa, kulimalizia, akasema, "Kama tukitenda dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Basi hiyo haina budi kuwa ndiyo dhambi isiyosameheka, ni, "kutenda dhambi makusudi." Je, hiyo ni kweli? "Atendaye dhambi kusudi."

121 Sasa, dhambi ni nini? Jambo lingine linalokubidi kujua, dhambi ni nini. *Dhambi* ni "kutotii." *Dhambi* ni "kukataa." Sasa angalieni hapa. Dhambi ya kwanza . . .

122 Nilikuwa na mahali hapa nilipotaka kuwaonyesha, mahali pa kwanza pa hii Scofield hapa, yale aliyoandika katika tanbihi hapa. Ninaamini inapatikana katika Warumi, mlango wa 3. Alisema hapa, kama alivyoifasiri kupitia Webster, bila shaka, katika tanbihi. Alisema, "Dhambi ni kukataa mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa."

123 Dhambi, katika umbo lake la awali, ni kukataa Neno la Mungu lililofunuliwa, lile ambalo Mungu . . . au mapenzi ya Mungu. Wakati Mungu amefunua kitu fulani kama mapenzi yake; basi kukataa Hicho, ni kukufuru, ama, kumkataa Mungu.

124 Dhambi ya kwanza ilikuwa ipi? Hebu tuiangalie. Rudini hapa katika Mwanzo 3. Mwaweza kulisoma mtakapofika nyumbani, mkitaka. Mwanzo 3, Mungu alipoweka bustani ya Edeni, akawaweka Adamu na Hawa mle, aliwaambia mambo ambayo wao . . . Hilo lilikuwa ni Neno Lake; Ambalo wangeweza kufanya, na mambo ambayo hawangeweza kufanya. Sasa angalieni wakati Shetani alipomjia Hawa, alisema, "Mungu amesema, 'Msile matunda yake,' lakini hakika hamtakufa." Mnaliona? Ndipo Hawa makusudi . . . Mnalipata? Hawa akifanya

kimakusudi jambo ambalo alijua kwamba Mungu alisema lisifanywe. Hiyo ni kweli? Sasa iangalieni. Wakati Hawa makusudi. . .Dhambi ya kwanza iliyopata kutendwa. Je, hiyo ni kweli? Hawa, makusudi, akijua mapenzi ya Mungu kisha akakataa kuyafanya. Hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo dhambi ya kwanza.

125 Basi dhambi ni nini? Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 3, kifungu cha 18, Yesu Kristo alisema, Mwenyewe, hivi, kwamba, "Asiyeamini amekwisha hukumiwa." Je, hiyo ni kweli? Basi kwa kweli dhambi ni kutokuamini.

126 Shetani, na katika ushawishi wake, alimwambia Hawa kwamba, "Mungu alisema hivyo, lakini hakulimaanisha." Unaona jinsi alivyolificha Neno? Naam, sasa alisema, "Sasa, Mungu alisema Hilo, bali Yeye hakumaanisha Hilo." Kwa maneno mengine, "Utakuwa. . .Macho yetu yatafunguliwa. Mtajua, mtakuwa na maarifa mengi zaidi."

127 Na sasa uwongo uo huo uliooza unasemwa na Shetani, kwa wahubiri na washiriki wa kanisa siku hizi, kusema, "Neno la Mungu linasema *hivi-na-hivi*, lakini halimaanishi Hivyo." Neno la Mungu humaanisha vile tu lilivyosema. Hiyo ni kweli.

128 Nilikuwa nikizungumza hapa, si muda mrefu uliopita, kwa kanisa langu na watu wangu mwenyewe, wakati wengine walipoliweka. . .walikuwa wametoka nje ya mji. Katika ibada za uponyaji, sijawahi kuwasilisha aina yoyote ya ma—mafundisho, kwa sababu limekuwa ni kundi lililochanganyikana. Lakini katika kanisa langu mwenyewe ninahubiri kile ninachoamini kuwa ni Kweli. Na yote ninayohubiri ni Kweli, bali siingii katika utondoti Wake. Mtu fulani aliponiona nikibatiza hapa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, walisema, "Ndugu Branham, nilifikiri ulikuwa wa—wa utatu, wakati wote."

129 Nikasema, "*Utashangaa* sana." Nikasema, "Biblia ilisema. . .Wala hakuna mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa njia nyingine yoyote ila katika Jina la Yesu Kristo."

"Vema," kasema, "lakini unajua. . . " Nikasema ninii. . .

Nikasema, "Kitu hicho kimewekwa moja kwa moja mbele zako."

130 Ndugu mmoja Mwadventista, ambaye, ndugu yake ameketi hapa sasa, alikuja hapa nyumbani kwangu wakati mmoja, kunisahi juu ya jambo lilo hilo. Ndugu yangu akamwambia, akasema, "Sasa, angalia, ndugu, unasikiliza jambo ambalo si kweli."

Naye akasema, "Kwani Bill Branham ni nani wa kuniambia?"

"Vema," kasema, "karibu ukasikilize Neno la Mungu."

131 Kwa hiyo huyo mvulana akaja, na tukafungua Biblia. Nikasema, "Sasa angalia, ndugu, utaweka kitabu chako cha kiada chini, na tuichukue Biblia?"

"Naam, Biblia."

132 Nikasema, "Basi kama Neno la Mungu likisema umekosea, utaniruhusu nikubatize katika Jina la 'Yesu Kristo'? Na kama ukinithibitishia kwamba 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu' ndiyo njia ya kubatizwa, katika Biblia, nitakuruhusu unibatize." Akakubaliana nalo.

133 Basi somo lake la kwanza likawa ndipo mahali pekee alipopata kufikia, naye akahukumika papo hapo, ndipo akakataa kuniruhusu nimbatize. Sasa hiyo ina maana gani? Yeye. . . "Tukitenda dhambi, au kutokuamini kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Hiyo hapo dhambi yako isiyosameheka.

134 Kama unajua Ukweli wa Injili ni nini, na umeelezwa kwako, na Mungu amekufunulia, nawe unajua ni Kweli; bali kuridhisha tu kusanyiko fulani au maskini mhubiri fulani, ama kuwa maarufu, kwamba unataka kushikilia mambo unayotaka kushikilia, badala ya kulichukua Neno la Mungu; Paulo alisema, "Atendaye dhambi au kutokuamini maksudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Hiyo hapo dhambi yako isiyosameheka, ni kujua kilicho Kweli na kukataa kutembea ndani Yake. Amina. Sasa, mnaamini hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. "Atendaye dhambi!" *Dhambi* ni "kutokuamini."

135 Vema, unasema, "Je, kuvuta sigara ni dhambi, kunywa pombe ni dhambi?" La, la. Hizo ni sifa za kutokuamini. Unafanya hivyo kwa sababu huamini.

136 Mtu akisema kwamba anaamini, hana budi kuwa Mkristo na kutembea katika njia anayosema ndivyo alivyo. Mnaona, sifa! Tofaa siyo mti; ni sifa za huo mti. Na kwa sababu unasema uongo, unaiba, unadanganya, na kuvuta sigara, na—na kufanya kila kitu, na kujiita Mkristo, ni kwa sababu hujazaliwa mara ya pili. Hiyo ni kweli. Hiyo inaonyesha kuwa hayo ndiyo aina ya maisha unayozaa. Yesu alisema, "Kwa matunda yao mtawatambua." Unaona?

137 Na kama ukifanya mambo hayo, Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia, ama mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako," wewe ni wa kidini tu na hujawahi kupata wokovu wowote. *Dini* ni kifuniko, lakini wokovu ni uhuru. Haleluya! Wokovu unafichua, hiyo ni kweli, na unaonyesha kile ulicho. Hiyo ni kweli. Sasa, sababu ya sisi kufanya mambo mabaya, ni kwa sababu hatuamini.

138 Lakini ikiwa unaamini kwa moyo wako wote kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Mungu anawajibika, ikiwa

ushuhuda wako ni wa kweli, kukupa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kukutia muhuri katika Ufalme hata Siku ya Ukombozi wako. Hiyo ni kweli.

139 Na kama ukisema, "Vema, nina Roho Mtakatifu! Utukufu kwa Mungu! Ninajua nimempata; nilianguka chini ya Roho." Loo, hiyo siyo dalili ya kwamba una Roho Mtakatifu, hata kidogo. Marafiki, nimeona vitu vya kila namna vikianguka chini ya roho. Hiyo ni kweli. Hilo halikufanyi uwe na Roho Mtakatifu.

140 Lakini unapokuwa na upendo wa Yesu Kristo moyoni mwako, Mungu anapokufanya Mkristo, anapokutia muhuri katika Ufalme Wake! Unaweza kuanguka chini ya Roho, pia. Unaweza kufanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*, chochote kile. Lakini maisha yako yatalingana na ushuhuda wako.

141 Maisha yako yanashuhudia kwa sauti kubwa sana, mpaka, haidhuru unasema nini, watu hawaamini ikiwa huyaishi. Hawatakuamini. Wala wewe huliamini, wewe mwenyewe, wala umma hauliamini, kwa hiyo unajifanya tu mwenye mashaka. Kwa nini usije kwa moyo wa kweli, na kusema, "Mungu, ninakiri makosa yangu, na ninamwamini Yesu Kristo kwa moyo wangu wote. Sasa, Mungu, nipe Roho Mtakatifu." Atafanya hivyo. Hiyo ni kweli. Atafanya hivyo. Basi, tunda la hilo, kwa sababu unaamini!

142 Sasa unasema, "Naam, niliacha kuvuta sigara. Niliacha kunywa pombe. Ni—niliacha kufanya *hili*, na *lile*, na *linginelo*." Ndugu, mwenye dhambi yeyote anaweza kufanya hivyo. Bila shaka, anaweza. Hilo halifanyi . . .

143 Katika ninii—katika wakati wa vita, umwone mtu, tuseme amevaa nguo rasmi za Marekani. Sasa, Ndugu Roberson, Ndugu Funk, wengi wenu ninyi askari hapa, msingeweza kumwamini mtu kwa sababu alikuwa amevaa nguo rasmi za Kimarekani. Huyo anaweza kuwa ni jasusi. Anaweza kuwa ni Mjerumani. Anaweza kuwa ni adui. Ati kwa sababu amevaa nguo rasmi za Kimarekani, hizo hazimfanyi kuwa Mmarekani. Hapana, bwana.

144 Haleluya! Unaweza kuwa mfuasi wa kila kanisa nchini, na ufungue kila ukurasa, kila Mwaka Mpya, na hilo halikufanyi kuwa Mkristo. Ndugu, unapokuwa na utambulisho wa alama ya vidole, basi wewe ni Mmarekani. Una hati ya utambulisho, kuthibitisha kwamba wewe ni Mmarekani.

145 Na unapokuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na Nguvu za Mungu zikifanya kazi maishani mwako, na kukufanya uishi kwa unyenyekevu na amani katika ulimwengu huu wa sasa, siku baada ya siku, juma baada ya juma, mwaka baada ya mwaka, wanajua unaposimama. Hiyo ni kweli. Daudi alisema, "Itakuwa kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji. Chochote afanyacho kitafanikiwa. Hatanyauka majira ya kiangazi, kwa sababu amepandwa kando ya mito ya maji." Naam, bwana. "Matunda yake hayatanyauka. Majani yake

hayatanyauka. Atazaa matunda yake kwa majira yake. Yeye... Sasa, sivyo walivyo wasio haki; wao ni kama makapi yakaukayo na kupeperushwa na upepo," hiyo ni kweli, kutoka uamsho mmoja hadi mwingine, nao inabidi waamshwe na kuamshwa. Lakini mtu aliyewahi kutia nanga ndani ya Kristo anajua alipo. Hiyo ni kweli.

146 "Sasa tukitenda dhambi," d-h-a-m-b-i, dhambi! Sasa dhambi ni nini? *Dhambi* ni "kutokuamini." Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Chukua kamusi yako ya Webster, popote unapotaka kwenda. Hapa katika Biblia, dhambi ya kwanza ilikuwa ni kutokuamini. Je, hiyo ni kweli? "Asiyeamini amekwisha hukumiwa." Kote katika Maandiko, kila kitu, ni "kutokuamini, kutokuamini."

147 Nikisema ni—ni usiku huko nje, kuna giza; ni kiasi gani cha giza, ni sehemu gani yake iliyo usiku? Yote ni usiku. Je, hiyo ni kweli? Ni usiku kwa sababu kuna giza. Hiyo ni kweli?

148 Je, nuru ni kiasi gani katika chumba hiki? Je, sehemu *hii* ni nuru? Naam, chote ni nuru. Ni nuru kwa sababu ni nuru.

149 Na kama wewe ni mwaminio, wewe ni Mkristo. Kama wewe si mwaminio, wewe si Mkristo. Hivyo tu.

150 Kwa maana huokolewi kwa matendo yoyote mema. Huokolewi kwa kupaza sauti. Huokolewi kwa kucheza katika Roho. Huokolewi kwa kunena kwa lugha. Huokolewi kwa kushika sabato. Huokolewi kwa kula nyama. Huokolewi kwa kujiunga na kanisa. Huokolewi kwa ubatizo wa maji. "Unaokolewa kwa imani. Kwa njia ya neema umeokoka." Vema.

151 Na kama umeokoka kweli, mambo haya mengine huja moja kwa moja. Unanena kwa lugha. Ungeweza kupaza sauti. Unaweza kumsifu Mungu. "Roho ya manabii huwatii manabii." Mchungaji akiona kitu kibaya, aseme, "Angalia, dada, ama ndugu, hilo ni kosa." Wewe ni mtiifu. Hiyo ni kweli. Wewe ni mtiifu. "Roho ya manabii humtii nabii." Anajisalimisha tu na kusema, "Mungu, nisamehe. Sikukusudia kutoka nje ya utaratibu. Niko tayari kuninii..." Loo, loo, kama kanisa lingesonga mbele, basi mtaliona kanisa likitenda kazi kwa utukufu wa Mungu. "Roho ya manabii humtii nabii." Kila kitu kiko katika utaratibu, kanisa limewekwa katika utaratibu.

152 Lakini kama ungewafanya wachomoze vichwa vyao, waseme, "Siamini! Nakwambia tu, siamini!" Hiyo inaonyesha papo hapo una kasoro. Hiyo ni makosa. Kuna kasoro. Huwezi kustahimili marekebisho. Unajua ninachomaanisha.

153 Maandiko yanasema, "Waangalieni hao," pia. Hiyo ni kweli, ikiwa huwezi kustahimili marekebisho. Huwezi kusimama kwa utaratibu. Huwezi kusimama katika mambo ya Mungu, kisha unajiondosha. Paulo alisema, "Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wa kwetu." Hiyo ni kweli. Kisha akasema,

"Mafundisho haya yote, na..." Tena akasema, "Ninapokuja kati yenu, kuna *hili*, na kuna *lile*, na kuna lingine." Kasema, "Naam, nasikia hata kuna ugomvi, na mtu mmoja anaishi na mama yake mzazi, na mwingine analewa katika meza ya Bwana." Kasema, "Ninasikia mambo haya yote. Hayapaswi kuweko." Ndipo walipoondoka, alisema, "Kweli, walitoka kwa sababu hawakuwa wa kwetu." Hiyo ni kweli. Alisema, "Mnakula kwenye meza za ibilisi, halafu mnakula kwenye meza ya Bwana, halafu mnajaribu kujiita Wakristo."

154 Aliwakemea. Aliwakatakata. Aliwapenda, lakini akawaambia Ukweli. Na wakati kizazi hicho kitakapofufuka, naye Paulo asimame mbele yao, Paulo angeweza kusema, "Sina hatia ya damu ya mtu awaye yote. Sikujiepusha katika kuwaambia Kweli yote ya Mungu."

155 Sitawajibika kwa ajili ya siku ya Paulo. Lakini kizazi hiki kitakapofufuliwa, itabidi nisimame kama shahidi. Basi, kama ninajua jambo fulani ni Kweli, kisha nikatae kulisema, na kupatana kwa sababu ya umaarufu, nitatupwa nje kama mnafiki. Lakini naweza kutupwa nje kama m—mdanganyifu, naweza kutupwa nje kama "mlokole," na kuitwa kila kitu duniani hapa; lakini Siku hiyo, Mungu anasema, "Umelishika Neno Langu, nitakulinda katika Siku ya Dhiki." Hiyo ni kweli. Hilo ndilo jambo la kufanya.

156 Kama Biblia haikufundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao ulikoma huko nyuma kabisa, ningefundisha jambo lile lile. Biblia inafundisha, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele."

157 Kama ikisema miujiza ilikoma pamoja na mitume, ningeamini. Lakini Mungu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao, hadi mwisho wa dunia." Ninaliamini.

158 Kama wakisema watu wangeweza kunena kwa lugha tu huko nyuma katika wakati wa mitume, nayo Biblia ilisema huo ulikuwa ndio wakati pekee ambao wangenena kwake, ningeiamini. Lakini Yeye alisema, "Ishara hizi, na kunena kwa lugha, zilikuwa ndani yake, moja kwa moja hadi mwisho wa ulimwengu."

159 Ikiwa ubatizo wa maji katika Jina la Yesu ulikuwa ukome pamoja na mitume; na katika mtindo wa kanisa Katoliki, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu;" kama tulipaswa kukoma kule nyuma, na kuanza na hili, ningefanya jambo lile lile. Lakini umefundishwa, ni ule ule, "Injili hii haina budi kuhubiriwa katika ulimwengu wote kwa ushuhuda, na ndipo mwisho utakuja." Ikiwa kunyunyiziwa kulikuwa katika Biblia, ningekuwa nikinyunyizia. Hiyo ni kweli. Chochote kile!

160 Kama kutawadha miguu hakukuwa katika Biblia, nisingeweza kukuhubiri. Lakini Biblia ilisema, "Heri ninyi

ikiwa mnajua mambo haya na kuyafanya." Nami nimesema Kweli.

161 Kama Meza ya Bwana ilikuwa ya kiroho, na haikupaswa kuliwa kikawaida, ningesema hivyo. Lakini Yesu alisema, "Heri . . . " Kasema, "Fanyeni hivi, na mle vipande Vyake, mwili Wake, mpaka atakaporudi tena." Nimesimama nalo.

162 Kama Yeye alisema, uponyaji wa Kiungu, Yeye alikoma kule nyuma, ningeamini. Lakini Yesu alisema, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya, hata mwisho wa dunia." Ninaamini Hilo! Kweli. Ninaamini katika ishara kuwafuata waaminio.

163 Ninasimama na kuona ulokole mwingi ukiinuka na uigaji, na kudhihaki na kufanya mzaha namna hiyo; sio kufanya mzaha, bali wanatoka nje na kuleta lawama, lawama kweli. Wanasimama kanisani na kunena kwa lugha, kisha wanatoka nje, na kukunja uso na kuzozana; na kuondoka, kwa ajili ya uamsho unaofuata, na kurudi ndani. Huyo si Mungu. Kweli. La, bwana. Kwa matunda yako unajulikana.

164 Sijali, basi, unaweza kuwasilisha Ukweli kwao, na kusema, "*Huu* hapa, BWANA ASEMA HIVI."

165 Ndipo mtu anaangalia Hilo; analiogopa. Naye anaondoka na kusema, "Loo, siamini Hilo, kwa vyovyote vile." Ndugu, umetenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu. Umefanya jambo ambalo hutasamehewa kamwe, mpaka utakapokuja kurekebisha jambo hilo.

166 Kama nikija mpaka Mto Ohio, na hapo kuna daraja, nao waniambie kuna daraja la kuvukia. Niseme, "Vema, nitaliendesha gari langu kwa njia nyingine." Hilo hapo daraja. Liliwekwa hapo. Kuna ushuru wa kulipa. Sina budi kuvuka hilo daraja, kama ninatarajia kufika Kentucky kutoka Jeffersonville. Sina budi kuvuka daraja hilo. Je, hiyo ni kweli? Loo, ninasema, "Sitafanya hivyo. Nitaenda tu nikajinunulie mashua, na kuvuka kwa mashua, ama nitamkodisha mtu." Sikilizeni, kuna haki ya usafiri kwenye daraja hilo. Unaposhuka kwenye ufuo wa pili, wenye mamlaka watakutana nawe papo hapo na kukukamata kwa kufanya hivyo. Hiyo ni kweli kabisa.

167 Si ajabu Yesu alisema, "Mtu mmoja aliingia bila vazi la arusi." Akasema, "Rafiki, unafanya nini hapa? Ni nani aliyekuleta humu?" Ndipo mtu huyo akasimama hajiwezi. Kwa nini hakufanya hivyo? Katika m- . . . katika huo mfano hapo.

168 Bwana arusi, katika nchi za Mashariki siku hizi, bwana arusi huandaa karamu ya arusi. Naye alipofanya hivyo, ni juu yake kutoa joho.

169 Yesu Kristo aliweka Karamu ya Arusi mwishoni mwa maisha, na ni juu Yake kufanya maandalizi ya hayo majoho.

170 Basi mlangoni, bawabu, tuseme, au mmoja wa marafiki zake wa karibu, alisimama pale. Na kila mtu aliyekuja na tiketi, alipata joho la aina ile ile. Walimvika. Ikiwa alikuwa amevaa matambara au kama alikuwa amevaa nguo za pamba, ni mamoja, alivikwa joho, bila shaka alionekana sawa kabisa na hao wengine. Hiyo ni kweli kabisa.

171 Na, ndugu, tutakapofika kwenye ile Karamu ya Arusi, hatuna budi kuvikwa vazi lile lile alilokuwa nalo Mtakatifu Paulo kule nyuma. Hatuna budi kuwa na ubatizo ule ule wa Roho Mtakatifu. Hatuna budi kuwa na Injili ile ile inayowaka moyoni mwetu, upendo ule ule, la sivyo tutakataliwa. Useme, "Vema, ndugu, nilikuwa Mpentekoste. Mimi. . . " La, bwana. Hiyo haitakuficha hata kidogo. "Nilikuwa Mmethodisti. Nilikuwa Mpresbiteri. Nilikuwa mfuasi wa Maskani ya Branham." Hilo halitakuwa na uhusiano wowote nalo. Hiyo ni kweli.

172 Unaona Ukweli wa Injili! Paulo alibatiza namna gani? Je, Kanisa la mwanzoni lilibatiza namna gani? Katika Jina la Yesu Kristo. Walifanya nini humo ndani? Walifundisha uponyaji wa Kiungu. Walifundisha Nguvu za Mungu. Walifundisha kule Kurudi hasa katika mwili. Walifundisha kushiriki kwa kawaida taratibu za kutawadha miguu na—na mkate wa ushirika, na vitu kama hivyo; wakamega mkate, nyumba kwa nyumba, kwa moyo mmoja. Hiyo ni kweli? Naam, bwana.

173 Waliamini katika kukemea dhambi mahali ilipokuwa, na kuweka mambo kando. Anania na Safira, haikuwa rahisi, lakini Petro aliwaambia, alisema kilichowapata.

174 Wakati maskini mchawi Simoni alipoamini, naye akaingia na kutaka kumnunua Roho Mtakatifu, ama kuwa mtu mashuhuri kanisani, kasema, "Nitaweka kiasi kikubwa katika hazina; acha nipite kwa vyovyote vile."

175 Petro akasema, "Pesa zako na ziangamie pamoja nawe." Wala hawakugusa vya kwake. Mungu awabariki watu hao waliokuwa na usadikisho halisi wa Roho Mtakatifu, kwamba waliona na kusema Kweli. Hiyo hapo. "Simoni, umekosea." Simoni alijua alikuwa amekosea.

176 Sasa kama ukikataa kutembea katika Hilo, unamkufuru Roho Mtakatifu. "Maana atendaye dhambi kusudi, baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

177 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ". . .usiibe. Usiseme uongo." Tulipitia hayo, asubuhi ya leo, tukaonyesha ya kwamba dhambi hata haikujulikana mpaka sheria ilipoikuza.

178 Kama vile sheria isingejulikana hapa mjini, haikuwa kosa kupita taa nyekundu, isipokuwa ilikuwa ni. . .kuna sheria dhidi yake. Kusingekuwako na sheria—kusingekuwako na sheria, ni

makosa kukimbia barabarani, maili tisini kwa saa, isipokuwa kuwe na sheria ya spidi.

179 Nasi tusingalijua dhambi isipokuwa kulikuwa na sheria. Basi sheria ilipokuja na kuikuza dhambi, au kuidhihirisha, ndipo neema ya Yesu ikaja na kuondoa tamaa ya dhambi moyoni mwako. Unaona, hilo liliondoa dhambi.

180 Kitu cha juu zaidi Mbinguni, Mungu Mwenyewe, kikawa kitu duni kabisa duniani, hata kikawakilisha nyoka. Je, mlijua hilo? Yeye alikuwa ni yule nyoka wa shaba nyikani. Je, hiyo ni kweli? Kutoka kwenye kitu cha juu kabisa cha Milele yote, hadi kiumbe cha chini kabisa duniani; na kutoka kwenye Kitu kitakatifu sana kilichokuwako, hata kile kisicho kitakatifu kilichokuwako, maana aliichukua dhambi ya kila mtu, kila mnyama, kila mwanadamu, juu Yake Mwenyewe, akafa kama mwenye dhambi, huku dhambi zako zikiwa juu Yake.

181 Nafsi ya pili isingeweza kuja, nafsi ya pili ya Uungu isingeweza kuja, nafsi ya tatu ya Uungu isingeweza kuja, nafsi ya nne. Malaika wasingeweza kuja. Mungu Mwenyewe alishuka, aliye juu sana, kufanywa duni kabisa, kuondoa dhambi.

182 Basi, wanaume kwa wanawake, angalieni alichosema, nanyi mumwamini. Sasa, Biblia, “Walipotenda dhambi makusudi.”

183 Yule mtu katika. . .alipokuja na kuweka mkono wake juu ya mwana-kondoo aliyekuwa akifa, alisema, “Nimefanya uzinzi, kuhani mkuu. Nami namtoa huyu mwana-kondoo asiye na ila,” mfano wa Kristo. Akaweka mkono wake juu ya maskini kichwa chake. Wakakata koo, naye akatetemeka na kulia na kufa, na kutikisika. Naye alijua ya kwamba mumo humo ndani mliwekwa dhambi zake. Anapaswa kufa namna hiyo, yeye mwenyewe. Ilibidi afe kama kibadala hiki kisicho na hatia hakikufa kwa ajili yake.

184 Kisha jina lake, Bw. John Doe, likawekwa kwenye kumbukumbu. Liliwekwa hapa. Mmoja wa Walawi aliliweka, vema, mwandishi. Aliwekwa hapa, basi, “Alikuwa amefanya uzinzi huu; alikuwa ametoa mwana-kondoo huyu kwa ajili yake.”

185 Kisha akatambua kwamba Neno la Mungu lilihitaji, “mara moja kwa mwaka,” hivyo tu. Vema, alirudi moja kwa moja akiwa na shauku iyo hiyo. Akamwona yule mwanamke tena, naye akazini naye tena; akaokota kuni siku ya sabato; vyovyote dhambi yake ilivyokuwa. Akarudi tena, na mwana-kondoo mwingine, kabla ya kutakaswa kwa madhabahu.

Ndipo aliporudi tena, “Jina lako ni nani?”

“John Doe.” Akainama akamwangalia John Doe.

“Kosa lako ni lipi?”

“Kufanya uzinzi.”

186 "Naam, tulimpata, tukamkamata kwenye hicho kitendo." "Mbona, tayari umelifanya. Umekuwa na upatanisho mmoja. Neno la Mungu linahitaji upigwe mawe." Ndipo wakamkokota kutoka mahali hapo huko, nao wakampiga mawe bila huruma. Sijali kama yeye ni meya wa mji, au alikuwa nani. Yeyote yule, alikufa bila rehema, hiyo ni kweli, kwa sababu alikuwa amelikataa Neno la Mungu. Mungu alihitaji mwana-kondoo mmoja, naye akakataa.

187 Na sasa Paulo alisema, "Hiyo ilikuwa chini ya sheria ya Musa. Yeye aliyeidharau sheria ya Musa, alikufa pasipo huruma, chini ya mashahidi wawili au watatu waliompata katika tendo hilo. Itakuwa ni zaidi sana vipi wakati mtu anapoweka kichwa chake juu ya Mwana-Kondoo wa Mungu, Mwana wa Mungu?"

188 Na moyo wake uliovunjika! Alichubuliwa. Huku machozi Yake yakitiririkia mashavuni Mwake; miiba juu ya taji Yake, huku damu ikitiririka juu ya uso Wake, iliyochanganyikana na machozi ya chumvi, hata kwenye mwili Wake ulio uchi. Ndipo mtu atakuja na kusema, "Naam, ninasadiki kwamba huyo ni Mwana wa Mungu," na kisha atageuka na kukataa kuamini neema Yake na rehema Yake na Neno Lake.

189 Paulo alisema, "Yeye afanyaye hivyo makusudi, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi, ila kuitazamia hukumu yenye kutisha na ukali wa moto utakaomla apingaye." Ndugu yangu, Ukweli unapowasilishwa kwako!

190 Ninaweka huu kama msingi wa kwanza kwa ajili ya uamsho ujao. Wewe leta Biblia yako kila usiku. Leta penseli yako, leta kitabu chako, upate kuangalia. Na wakati wowote unapoona chochote usichoelewa, "njoo, tusemezane."

191 Nataka kujua Ukweli, pia. Mimi niko wazi tu kupokea Ukweli kama wewe ulivyo. Nami nataka kujua lililo kweli na lililo uongo, kwa maana sitaki kukosa kutii jambo moja ambalo Yeye alisema lifanywe. Mnaona? Ninataka kila sehemu Yake katika moyo wangu mwenyewe, bali haina budi kuja kwa Neno. "Kwa maana tukikosa kuamini makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

192 Hebu niingize hili, katika kufunga, katika dakika moja tu. Angalieni. Sasa, wakati, Yesu aliwaambia walikuwa wamemkufuru Roho Mtakatifu, ambayo haikuwa... isiyosameheka—dhambi isiyosameheka.

193 Tazama, nabii Isaya, wote, Yeremia, manabii wote, walisema, "Ajapo Masihi, huyu angekuwa Ndiye." Mungu... Yesu Kristo alikuwa Neno la Mungu. Je, hiyo ni kweli? Kumkataa ni kulikataa Neno. Hiyo ni kweli?

194 "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Na *Hapa* lilikuwepo Neno

la Mungu lililoandikwa likidhihirishwa hapa, kama Neno la Mungu duniani. Kila Neno Lake alilonena lilikuwa ni Biblia. Kila aya aliyowazia ilikuwa ni neno lililoandikwa. Alikuwa Neno la Mungu. Ndipo wakati. . . Neno lililoandikwa lilikuwa limetangaza ya kwamba Yeye alikuwa Neno. Ndipo wakati alipokuja akidhihirishwa hapa duniani, nao watu wakaliangalia Neno na kulikataa, mnaelewa ninachomaanisha? Kwa sababu walipoteza heshima yao, kwa sababu iliwabidi kuliacha kanisa lao.

195 Mtu yeyote alisema, "Kama ukiamini uzushi wa aina hiyo, tutakuondosha kanisani." Vema, hawangeweza kumwamini. Walimwamini, moyoni mwao, ila hawakumtaka. Hawangethubutu kuungama hadharani, kwa sababu, kama wangefanya hivyo, wangefukuzwa kanisani mwao. Kwa hiyo, "Walipenda sifa za wanadamu kuliko sifa za Mungu." Walisema, "Vema, kanisa letu halilifundishi hivyo hasa, kwa hiyo tutaninii tu. . . "

196 Waangalie hao mashetani wa kale wakiishi leo. Hakika. Wanaishi leo. "Vema, mama yangu alikuwa Mkatoliki. Na mama yangu alikuwa Mpresbiteri. Nami nakwambia, yeye, alikuwa mama mzuri. . . "

197 Mama alitembea katika nuru aliyokuwa nayo, lakini siku imewadia ambapo Nuru ya Injili inaangaza. Theolojia ya ka-. . . Makanisa ya Kikristo yanakufa. Yameshindwa. Mungu anakuchukua sasa, ili ajifunue Mwenyewe tena, kupitia Kanisa Lake, Mwili uliofufuka wa Bwana Yesu Kristo. Uliofufuliwa kutoka kwa ukanisa; uliofufuka kutoka kwa makanisa rasmi baridi; uliofufuka kutokana na ulokole. Mungu analeta fungu la mifupa na kuitia ngozi, katika Uweza wa Roho Mtakatifu utakaoleta Injili katika siku hizi za mwisho, pamoja na ishara na maajabu, hata mwisho wa dunia. Watafundisha Biblia. Watasimama Nayo. Wataishi kwa Hiyo. Hawatapatana, kulia wala kushoto. Kweli. Watasimama moja kwa moja kwenye Neno, na kusonga mbele. Naye Mungu atakuwa pamoja nao, kila siku, akilithibitisha Neno, kwa ishara na maajabu yanayofuata. Haleluya! Enyi nyote nyota za asubuhi, amkeni mkaangaze! Haleluya!

198 Yule pale juu ya mnara wa ulinzi. Ndipo akasema, "Loo, mlinzi, habari gani za usiku?" Akasema, "Usiku unakuja. Na asubuhi inakuja, pia." Tazama, kila wakati usiku kabla ya asubuhi. Hiyo ni kweli. Walijua wakati kwa nyota. Na yapata tu wakati ilipofikia, mahali fulani kabla ya mapambazuko; nuru ilikuja, inasukuma giza mpaka, wakati wa giza sana uliopo, inakuja nuru. Giza kabla tu ya mapambazuko.

199 Ikiwa wewe ni mtu mzoefu wa milima. Naam. Sijali upepo unakuja kwa njia ipi, jinsi unavyokuja, jinsi unavyovuma sana. Acha miale hiyo ya kwanza ya nuru ichomoze angani kule,

nao upepo utashuka moja kwa moja kwenye mkondo, uje moja kwa moja kupitia bondeni. Sijali huo upepo unaovuma ni wa aina gani, utasimama moja kwa moja kwenye mapambazuko, na kushuka kwenye huo mkondo. Loo, haleluya!

200 Ndugu Funk alikuwa amelala kule hivi majuzi usiku, mimi na Ndugu Roberson, na hao wengine. Nikatoka pale nje, nikavaa viatu vyangu. Nikaanza tu kulia, nikarudi mbio hemani. Nikapata ufunuo, nikisimama pale. Nikarudi ndani ya hema, naye Ndugu Wood alikuwa amelala pale, amelala fofofo. Nami nilikuwa nimeketi pale, kando ya mahali pale, nikilia tu kwa nguvu niwezavyo, nikitetemeka, kwa maana niliona jambo fulani. Nikasema, "Naam, Bwana, usiku waja. Na mchana unakuja, pia."

201 Tunapitia wakati mkuu wa kukandamiza, wakati theolojia na kila kitu cha makanisa, iliyosema, "Njoo, ujiunge na letu. Njoo, ujiunge na letu. Njoo, ujiunge na letu." Lakini inapoanza tu kupambazuka, Upepo huo wenye nguvu unaoenda kasi unashuka kwenye huo mkondo tena, moja kwa moja kuingia Kanisani namna hiyo, wakati tu wa mapambazuko. Loo, lazima iwe ni mapambazuko ya siku, haleluya, kwa maana Nguvu zile zile za Roho Mtakatifu zinatangaza Injili ile ile iliyokuwako hapo mwanzo. Zimeitangaza tena leo. Haleluya! Loo, jamani! Nina furaha tunatembea kuelekea Sayuni, Kanisa la Mungu aliye hai. Haleluya! Ninaamini.

202 Mnafikiri nina kelele? Nina kitu cha kupigia kelele, hebu niwaambie, ndugu yangu, wakati Damu ya Yesu Kristo inaposafisha dhambi zote. Nimeona miaka ishirini na mitatu sasa, ya uongozi wa Roho Mtakatifu, kujisalimisha Kwake, na kutokuzingatia chochote kile ambacho hakisemi kitu. Imeweka kitu fulani moyoni mwangu, ambacho kimetiwa nanga mle, ambacho sikukiweka, mimi mwenyewe. Roho Mtakatifu alikiweka mle. Mungu anayo Kweli kwa ajili yangu. Nitatembea Nuruni kama Yeye alivyo katika Nuru. Nitakuwa na ushirika, mmoja kwa mwingine, huku Damu ya Yesu Kristo ikitakasa kutokana na udhalimu wote.

203 "Maana atendaye dhambi makusudi, anayekataa makusudi, baada ya kuona ufahamu wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

204 Sikilizeni hapa, wanaume kwa wanawake, sasa; marafiki zangu, na marafiki Wakristo. Kama jambo pekee unalojua ni kuja tu kanisani, acha hilo sasa hivi. Acha kudhania tu kuwa uko sawa. Kama una nia ya mawazo tu, "Vema, ninaamini nimeokoka," na unaona kwamba sikuzote unaleta ugomvi, au sikuzote unanung'unikia jambo fulani, una kasoro; ukiona huwezi kuondoa uadui moyoni mwako, ukiona kuna kitu kama hicho.

205 "Usidanganyike; Mungu hadhihakiwi." Hiyo ni kweli. "Chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." Hiyo ni kweli. Jambo likupasalo kufanya . . .

206 Unasema, "Vema, ninaamini nina Roho Mtakatifu," nawe unaona hazai matunda ya upole, na kujitolea, na—na wema, na upole, na msamaha, na kadhalika, basi ni wakati wako wa kujitikisa.

207 "Kwa maana kama ukitenda dhambi makusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki dhabihu tena kwa ajili ya dhambi," mpaka utakapokuja na kulisahihisha jambo hilo. Hiyo ni kweli. Ikiwa unajua unafanya makosa; nenda moja kwa moja kwa unyenyekevu uwezavyo, lichunguze.

208 "Vema," unasema, "Nitalichunguza, baadhi ya siku hizi." "Baadhi ya siku hizi" inaweza ikawa ni muda mrefu sana. Unaweza usiishi "baadhi ya siku hizi." Jambo la kufanya ni kulichunguza sasa hivi. Hiyo ni kweli. Lichunguze uone kama ni kweli. Na kama ni Kweli, ingia ndani Yake, na Mungu atakubariki.

209 Hebu niwaambie jambo moja kabla . . . katika dakika moja tu sasa, kabla hatujafunga. Samahani kuwawekeni hivi, lakini hebu niwaambie tu baadhi ya mambo ninayojua. Ikiwa kuna kitu chochote ambacho ninachangia kwa ujasiri kutembea mbele za mambo, ninapojua kwamba mambo fulani-fulani ambayo yanakuja kutoa changamoto wakati huo, mbele ya pepo na mamlaka. Kuna jambo moja ambalo ninaweza kusimama juu yake, na nijisikie vizuri; mambo mawili, hasa. Jambo moja, ambalo, ninajua kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu, nimejaribu kulifundisha Neno jinsi lilivyosema hasa. Ninajua ya kwamba Mungu aliahidi angeliheshimu Neno hilo. Sijali ni nini kinacholihubiri, linatoka kwa kitu gani, kama linatoka kwa mnafiki, Mungu ataiheshimu ile Kweli. Mnaamini hilo? Sijali kama ndiye mnafiki mkubwa kuliko wote ulimwenguni, Mungu ataiheshimu ile Kweli. Hiyo ni kweli. Ninajua ya kwamba Hii ni Kweli, kwa maana nimeisoma kutoka katika Biblia hii. Ninajua hiyo ni Kweli. Na jambo la pili, basi, ninalojua, Malaika yule, alipokutana nami pale, alisema, "Usiogope, nitakuwa pamoja nawe." Hiyo ni kweli.

210 Na, kwa hiyo, bila kujua vipi, nalitoka bila maono, mbele ya mambo, bila kujua la kufanya. Ninapopata ono najua la kufanya. Lakini wakati Yeye haniambii, na inanibidi nitoke huko nje moja kwa moja, na changamoto kwa uovu. Papo hapo, nawazia, "Bwana, sikujiepusha, bali nilitangaza mashauri yote ya Mungu. Kila kitu katika Biblia hii ulichosema kifanywe, nimejaribu kukifuata. Kwa hiyo, Bwana, moyoni mwangu mnakaa Neno Lako. Unawajibika kuliangalia Neno Lako. Kama kuna jambo lolote ninalojua kwamba napaswa kufanya, na sijalifanya,

Bwana, limefichika kwangu. Ninajua nimejaribu kutembea na Wewe, na ninajua umeliheshimu, na yote."

211 Nami nimewaambia watu, ingawa inaniudhi vibaya wakati mwingine, kuwaambia watu; bali nimewaambia, hata hivyo, kwa kuwa ni Neno. Wala kamwe sitawaambia walifanye, isipokuwa nilifanye mwenyewe. Naam.

212 Nikaja namna hiyo. Kisha ningetembea karibu kidogo, nami nawazia, "Bwana . . . " Kuona hizo nguvu zikisimama kule, huyo pepo akiwa tayari kukupa changamnoto, na kukusahi umkaribie. Nasema, "Bwana, si neno langu; ni Lako ninasimama juu yake sasa." Nikaenda pale, nikichukua wakati wangu.

213 Ninafika huko, nawazia, "Ee Malaika wa Mungu, Uwepo Wako na ukaribie, kwa maana Wewe ni mtumishi Wake ambaye alitumwa kunilinda katika saa hizi. Nawe uliniahidi huko, kama ningeenda, ungekuwa pamoja nami."

214 Kwa hivyo ninaenda moja kwa moja huko, na kusema, "Basi, katika Jina la Yesu Kristo, ninasema Kweli." Nawaangalia pepo wakipiga mayowe, naangalia mambo yakitendeka, kwa sababu Mungu anawajibika kwa Neno Lake.

215 Lakini kama ningejua mambo haya ni kweli, kama mabatizo, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na shughuli hizi zingine zote na kadhalika, na kujua zilikuwa ni Kweli, na kwa sababu tu nilitaka kuwa maarufu miongoni . . . na mtu anipigepige mgongoni na kusema, "Daktari, Mchungaji, au—au Askofu," au chochote kile, "u—u—u—ulihubiri mahubiri mazuri." [Ndugu Branham anapigapiga kitu fulani mara kadhaa—Mh.] Hiyo ndiyo sifa ya mwanadamu.

216 Ni afadhali wawe wananibeza na kunicheka, na kunidhihaki kwa kila njia, na kujua kwamba nimesimama mkweli kwa Mungu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sitaki sifa za wanadamu. Nataka sifa za Mungu. Ninataka kujua ya kwamba sijakwepa kuitangaza ile Kweli. Basi kama ukiikataa, hiyo ni juu yako. Unaona? Hiyo ni kweli.

217 Lakini hebu niwaambie Kweli ya Injili sasa, katika uamsho ujao. "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hataingia kamwe katika Ufalme," Maneno ya Yesu Kristo, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 3. Alimwambia yule mtawala mkuu. Huyo alikuwa mtu wa dini. Alikuwa mtu mashuhuri. Alikuwa mtauwa. Alikuwa mwalimu. Alikuwa mwanachuoni. Kila kitu ambacho ungeweza kutarajia ndani yake, alikuwa. Lakini Yesu akamwambia kwamba hakuwa na Uzima wa milele, maana hakuwa amewahi . . . Hata hakuelewa Hilo. Alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili," vema, "hawezi kuuona Ufalme wa Mungu," haidhuru alikuwa wa kidini jinsi gani. Alikuwa mfuasi wa kanisa lililo kubwa kuliko yote. Alikuwa na moja ya majina makubwa kuliko yote. Alikuwa mwalimu wa Biblia,

lakini hata hivyo hakuwa ameshuhudia tukio la Kuzaliwa upya. Je, unao, usiku wa leo?

218 Ninataka kuwaulizeni swali, waziwazi, kinaga ubaga. Sisemi ili kuwaaibisha. Afadhali niaibike hapa kuliko kuaibika Huko. Si ni afadhali ufanye hivyo? Kuna wengi wenu hapa ambao wanatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu.

219 Wengi wenu hapa mmeniangalia tangu nilipokuwa mvulana, mtoto mdogo tu hapa, ama katika umri wangu wa utineja, nikihubiri Injili. Wala sijabadilika hata chembe moja kutoka kwa Injili niliyoanza nayo. Bado ninafundisha kitu kile kile. Kwa sababu, sikupewa na seminari fulani, wala haikufundishwa na mwanadamu. Ilikuja kwa ufunuo wa Biblia. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, ninajua ilitoka kwa Mungu, nami nimedumu na Injili iyo hiyo.

220 Miaka mingi iliyopita, nilihubiri ubatizo wa maji kwa Jina la Yesu Kristo. Miaka mingi iliyopita, nilihubiri utakaso wa nafsi ya mwanadamu kwa Damu ya Yesu Kristo, kupitia utakaso. Nilihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu kama thibitisho, ama kutiwa muhuri kwa watu wa Mungu, katika Ufalme. Mnajua hiyo ni kweli. Nimefundisha uponyaji wa Kiungu. Nimefundisha Kuja mara ya pili. Nimefundisha kutawadha miguu. Nimefundisha ushirika. Nimefundisha utakatifu mbele za Bwana. Nimefundisha mambo hayo yote, kwanza kabisa.

221 Nilifundisha kunena kwa lugha, "si ushahidi wa Roho Mtakatifu." Nimefundisha kupaza sauti, "si ushahidi wa Roho Mtakatifu." Hakuna mojawapo ya mambo hayo unaloweza kusema ni ushahidi wa Roho Mtakatifu, ama ushahidi pekee. Huenda ikawa ni ushahidi kwamba Roho Mtakatifu yuko mle. Kuimba kunaweza kuwa ushahidi kwamba Roho Mtakatifu yupo. Kuzungumza kunaweza kuwa ushahidi kwamba Roho Mtakatifu yupo. Yoyote ya hizo ishara inaweza kuwa, na bado si kwamba haiwezi kukosea. Kuna Mtu mmoja tu ambaye anaweza kusema Roho Mtakatifu yuko mle, huyo ni Mungu Mwenyewe. Yeye ndiye Mwamuzi. Nimewaona wakiimba, nimewaona wakizungumza, nimewaona wakipaza sauti, nimewaona wakinena kwa lugha, na mambo hayo yote, wala hawakumpokea. Matunda yao yalithibitisha ya kwamba hawakuwa Naye.

222 Una imani yote, nadhani, nami, kuamini ya kwamba ninaye. Mimi pia. Mimi . . . Mungu anajua. Ninaamini ya kwamba unaye. Nina imani yote kwako, kuamini hilo. Wewe ni mkarimu, mwenye upendo, na mtamu, na kila kitu. Ninaamini kwamba ninyi ni—ninyi ni Wakristo. Ninaamini ya kwamba mna Roho Mtakatifu. Nisingeweza kuliapia. Mungu anajua hilo. Hiyo ni kweli, mnaona, kwa hiyo hatuwezi kuamua kwa mambo haya. Huwezi kumbana Mungu na kusema "*hii* Ndiyo," kwa sababu

Yeye Ndiye Mwamuzi. Hatukutumwa kuhukumu. Tulitumwa kuhubiri. Je, hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli, kuhubiri!

223 Nami ninaweza kuileta Kweli. Kama ukiikataa na kuondoka, ninajua Biblia inasema, ukifanya hivyo, basi wewe. . . Hakuna ondoleo la dhambi tena mpaka utakapokuja kurekebisha hilo tena. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo, ukiiona Kweli, tembea katika Kweli.

224 Na sasa, mnapokuja, ninataka kuwauliza jambo fulani. Ni wangapi hapa, wanasema, "Ndugu Bill, moja kwa moja, dha—dhahiri tu kadiri niwezavyo mbele ya umma, kwamba huenda nikafa kabla hata sijatoka katika jengo hili, bali nataka Mungu ajue na watu wajue hapa, kwamba ninataka ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu"? Je, unaweza kuinua mkono wako, useme, "Kweli nataka sana ubatizo wa kwe-. . . "? Mungu akubariki. Sasa tumepata nafasi ya uamsho.

225 Basi sikilizeni, enyi marafiki, msije, mkisema, "Vema, sasa, kama ninajisikia baridi sana, na—na kama nikimpata jinsi dada alivyompata. . . " Jinsi vile dada alivyompata, usimtafute hivyo.

226 Njoo tu kwa moyo safi, ukiamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwokozi, nawe umemkubali, nawe unaamini Mungu atalitimiza Neno Lake, nawe unatazamia kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, Naye atakupa. Useme, "Bwana, nitaninii. . . Kwa njia yoyote tu Wewe mmwage ndani yangu, bora tu nimempata Roho Mtakatifu. Hilo tu ndilo ninalotaka, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nipe Kitu kitakachoondoa huu ubinafsi. Nipe Kitu kitakachoondoa woga huu wote na mashaka. Jamani, Bwana, usinifanye. . . Ukinifanya nipaze sauti; nimeona wengine wakipaza sauti, wala hawakuliishi. Usinifanye ninene kwa lugha; Bwana, nimeona wengine wakinena kwa lugha wala hawakuliishi. Lakini, Bwana, weka Kitu ndani yangu ambacho kitaishi ndani yangu, ambacho kitanifanya nitembee kila siku kama Mkristo. Ambacho kitanifanya niwapende adui zangu. Ambacho kitanifanya ninene mazuri juu ya wale wanaoninena mabaya. Ambacho kitanifanya niwe tayari kutubia chochote kibaya ninachofanya, nije moja kwa moja na kukiri. Nitasema, 'Nimekosea. Nisamehe, Mungu.'"

227 Hiyo ndiyo aina ya roho unayotaka, sivyo? Naam, bwana. "Nifanye mnyenyekevu. Mchungaji wangu akiona kitu kibaya ndani yangu, anakuja na kusema, 'Sasa, ndugu, ama dada, hupaswi kufanya mambo haya.' Nifanye mnyenyekevu, niseme, 'Naam, ndugu yangu, nisaidie sasa kuomba. Sitaki roho ya aina hiyo juu yangu. Sininii. . . '" Hutaki roho ya aina hiyo, sivyo?

228 Hutaki kuzunguka ukiwa na kiburi, ukisema, "Kweli, a-ha, hakustahili kuniambia. Ninajua mahali ninaposimama." Loo, mnapofanya hivyo, enyi marafiki, mnaweza kuona papo hapo ya kwamba mko nje ya mapenzi ya Mungu. Mnaweza kuona mmekosea, kwanza kabisa.

229 Kwa nini usiwe mnyenyekevu, na kujitiisha kwa Roho Mtakatifu, useme, "Naam, nitavaa silaha na kanisa zima la Mungu aliye hai. Nitaendelea mbele. Nikiona jambo baya kwa dada yangu, nitamwombea. Nikiona kitu kibaya kwa ndugu yangu, naenda . . . Ikiwa ataendelea mbele, nitaenda nyumbani kwake na kusema, 'Ndugu mpendwa, naomba niushike mkono wako kwa dakika moja. Je, unanipenda?' 'Naam, nakupenda.' 'Unajua, tu—tunazeeka nasi . . . ' Hataki kwenda katika kuzimu ya ibilisi. 'Nami nimeona ukifanya jambo fulani. Sasa hebu—hebu mimi na wewe tuliombee.'" Mnaona, kitu kama hicho.

230 Ndipo basi kama huyo ndugu hatakupokea, basi huwezi kusaidia jambo hilo. Basi chukua ndugu mwingine mwende naye. Ndipo akishikwa na kiburi, basi umefanya wajibu wako, hivyo tu. Basi nenda kaliambie kanisa, na hilo latosha, unaona.

231 Sasa, unajua vizuri sana, na kundi hili dogo la watu wanaoketi papa hapa, umeuona mkono wa Mwenyezi Mungu juu ya mambo hayo. Unajua watu ambao wametembea papa hapa, waliodai kuwa na Roho Mtakatifu. Unajua hilo. Nao walipanda kuja hapa wakashikwa na kiburi, na kutojali, na chochote kile, kisha wakaondoka.

232 Niliporudi, mchungaji aliniambia, hivi majuzi usiku. Kasema, "Ulienda kumwona?"

"Naam."

"Ulichukua mtu mwingine?"

"Naam."

233 Nakumbuka wakati Ndugu Shelby akiniambia kuhusu . . . Na hao wengine, watu mbalimbali waliowaendea hao watu, wakijaribu kuninii . . . Niliwaendea hao watu. Nikasema . . . Loo, jamani, walinidhihaki na kusema kila kitu. Wakaniita kila kitu. Nikasema, "Sasa, angalia, rafiki yangu mpendwa, hili halitafaa kitu."

234 "Loo, jamani, umetoka tu ulimwenguni, nawe umerudi nyuma. Nawe uko *hivi*, wala huwaleti watu wakaokoke, na yote namna *hii*. Na yote unayowazia . . . "

235 Nikasema, "Hivi huoni kwamba ninamfuata Roho Mtakatifu, aongoze?"

236 "Loo, umekosea! Wewe ni *hiki*, *kile*, na *kinginecho*. Inakupasa kunitii! Mimi ndiye ninayekwambia la kufanya!"

237 Ndipo unaona papo hapo basi ni ibilisi. Kisha nikasema, "Angalia, tangu sasa na kuendelea, kama hutapatanishwa na kanisa; wanakupenda, lakini ikiwa hutarudi, basi kumbuka . . . Nimekuwa kwenu mara nne au tano, kila mmoja wenu. Kisha pia nimewaambia, nikaja na wengine, wala hamngepatanishwa. Sasa nitalielezea mbele ya kanisa, na, tangu sasa na kuendelea, hamna budi kuwa kama mpagani na mtoza ushuru." Hilo ni

Neno la Mungu, haidhuru linasikika kali jinsi gani. Hilo ni Neno la Mungu.

238 Kisha nikaenda kanisani, nikasema, “Tangu sasa, watu hawa si ndugu na dada zetu, kwa sababu wamejitenga nasi, inaonekana hawana Roho, nao wametoka, nanyi mnaona kilichotukia.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, mnaona kile kilichotokea.

239 Huwezi kulikwepa Neno la Mungu. Mungu anaposema ufanye jambo fulani, ndivyo hasa Mungu anamaanisha ufanye. Hiyo ni kweli.

240 Kwa hiyo sasa tuungane pamoja. Hebu na tuwe kundi la watu hapa, katika maskani hii ndogo, si kwa sababu . . . Mkitaka kuliondoa hilo jina langu pale mbele, hilo . . . Waliliweka tu hilo hapo. Iiteni tu chochote mtakacho. Mimi . . . haileti tofauti yoyote. Mnaweza kuiita tu “kanisa,” mkitaka. Sio lazima iwe maskani ya “Branham.” Branham hana uhusiano wowote nayo, hata kidogo, hata kidogo. Waliweka tu jina langu pale kwa sababu hatimiliki ilikuwa katika jina langu pale, nao wakaituma.

241 Nami nikashuka kule na kufanya kazi wakati wa kuzorota kwa uchumi, na—nao wakaleta zaka zao. Badala ya mimi kuzichukua na nisifanye kazi, nilitoa zaka zangu mwenyewe, na matoleo yangu, na pesa zikachangwa, nasi tukaijenga hii maskani hapa. Nayo imejengwa kwa matoleo niliyopewa na watu, kwa ajili ya riziki yangu. Nilifanya kazi na kuzirudisha maskanini, na hiyo ndiyo sababu wanaiita Maskani ya Branham. Hilo halina uhusiano wowote nayo. Kama ikiitwa maskani ya Neville, iitwe chochote mtakacho, haileti tofauti yoyote. Ni sehemu ndogo tu ambayo Mungu ametupa sisi kuviweka vichwa vyetu.

242 Na hapa ndani tunakuja na kumwabudu Bwana, kuifundisha Biblia kweli tu jinsi tujuavyo. Ndugu, imeshutumiwa katika mataifa yote, mahali pengi katika kila namna ya jambo, na hata hivyo Neno la Mungu linasonga mbele vivyo hivyo, safi tu, na kamilifu, na lisiloghoshiwa, liwezavyo kuwa. Njoo ujiunge nasi sasa; sio kujiunga na kanisa, sio kujiunga nasi. Lakini njoo ujiunge ndani ya Yesu Kristo. Umpende Yeye. Na kama Mungu ameliheshimu sana Neno Lake, kuwaponya wagonjwa, na vi—vipofu, na wanaoteseka, na kulitangaza kote ulimwenguni, hakika Yeye asingeniruhusu nitoke na kosa basi, sivyo? Na . . . ? . . . Wakati likiwa papa hapa, limeandikwa katika Neno la Mungu, msilikatae, ndugu zangu. Lipokeeni, kwa maana ni Bwana Yesu.

243 Basi, ninyi nyote, pokeeni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hebu tuwe familia moja kubwa yenye furaha. Basi usiingie, ukisema, “Vema, nina Roho Mtakatifu; utukufu kwa Mungu, nitapata karama sasa!” Achaneni tu na karama; zitajishughulikia

zenyewe, mnaona. Mungu, anapoona anataka kukutumia kwa jambo fulani, atakwambia la kufanya, nawe uende ukalitekeleze. Msizitafute karama. Mtafuteni Mpaji. Ingieni mkampokee Roho Mtakatifu. Ninaamini tutakuwa na wakati mzuri sana, sivyo na nyinyi?

244 Sasa, dhambi isiyosameheka ni ipi? Ni kufanya dhambi makusudi, baada ya kuupata ujuzi wa ile Kweli. Je, hiyo ni kweli? "Kwani yeye atendaye dhambi . . . " Nayo dhambi ni nini? Kutokuamini. Unapolitazama na kusema, "Hiyo ndiyo Kweli," bali unakataa kuipokea. "Atendaye dhambi, au kutokuamini, makusudi, baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Hiyo hapo Kweli. Hiyo hapo imewekwa. Na ni kama tu vile unavyokuja . . .

Hili hapa jambo lile lile katika njia kuu. Hebu tuangalie. Nitafunga basi.

245 Huyo hapo Yesu Kristo, Yeye ni Mwana wa Mungu; kumkubali ni Uzima, kumkataa ni mauti. Fanya utakacho. Unasema, "Vema, sasa, siamini Hilo. Vema, nawaambia, siamini Hilo. Kabisa siliamini." Naam, endapo huliamini, hiyo ni juu yako; huna Uzima, hayo tu. Kwa sababu, Hiyo ndiyo Kweli. Hiyo ni kweli. Vema.

246 Jambo lile lile kwenye Ukweli mwingine wowote. Hiyo ni kweli. Kukataa, kukanusha, kutoliamini Neno la Mungu, ni dhambi isiyosameheka. Huna haki zaidi. Kama ukipanda na kusema, "Vema, siamini Yeye alikuwa Kristo," basi hutaokolewa kamwe mpaka utakapolitubia na kupatanishwa Kwake. Unasema . . . Hii ndiyo Kweli ya Mungu, nayo imeelezwa kwako, nawe unasema, "Loo, siiamini Hiyo," basi umetengwa na Mungu mpaka utakapotubu na uje kwenye ile Kweli. Hiyo ni kweli?

247 Bwana mwema na awabariki sana. Na awadumishe katika afya njema.

248 Niombeeni wakati nimeondoka, (mtafanya hivyo?) kwamba Mungu atanipa usalama, na kurudi tena kwa ajili ya uamsho. Na, basi, juu ya msingi huu wa Kweli ya Mungu iliyoandikwa, tunaanzisha uamsho unaokuja. Mungu na awabariki tunapoinamisha vichwa vyetu.

249 Ndugu Teddy, kama utakuja hapa kwenye piano kwa muda kidogo tu, tupe wimbo mdogo tu wa namna fulani, tukiwa katika maombi sasa.

250 Baba, mafundisho hayo marefu, ya muda mrefu, makali, yenye kukata; kumhisi Roho Mtakatifu akiingia kwanza kwenye mkutano na kutupa baraka, kwamba Yuko hapa, mwanzoni mwa haya mafundisho. Tukijua kwamba alikuwa hapa! Kisha kuwazia, kuliendea Neno, kufikia hoja nzuri sana

ya jinsi dhambi isiyosameheka ingekuwa, ingekuwa. . .kutotii au kulikataa Neno la Mungu.

251 Kisha, Baba, tunaliangalia hilo, na kuwazia, "Ee Mungu, nitakase na kutokuamini kote. Jalia niamini ya kwamba Biblia hii ni Neno Lako. Jalia niamini ya kwamba imeandikwa hapa kwa ajili ya pongezi na marekebisho, ili mtu apate kusimama mbele za Mungu, bila hatia, akijua ya kwamba tutahukumiwa kwa Kitabu kiki hiki."

252 Naye alisema, "Heri anayeyashika maneno ya Kitabu hiki na kuyafanya. Huyo atakuwa na haki ya kuuendea huo Mti wa Uzima. Lakini wale wasioyafanya, watahesabiwa kuwa mbwa na wachawi, na kadhalika, ambao watatupwa nje, ambao mwisho wao ni kuchomwa moto. Heri ayashikaye maneno hayo. Naye atakayeondoa kwenye Kitabu hiki, aweke kitu kingine mahali Pake, huyo ataondolewa, jina lake, katika Kitabu cha Uzima. Lakini kila atakayezishika amri hizi zote, na kuyafanya mambo haya, atakuwa na haki ya kuuendea huo Mti wa Uzima."

253 Mungu, jalia, ya kwamba mimi, sisi katika kanisa hili usiku wa leo, daima tutatembea katika Nuru ya Biblia, na tutafanya tu yale ambayo Biblia inasema; pasipo kuangalia kulia wala kushoto, au kutokuamini. Jinsi Neno Lako lilivyo, ni Kweli. Tusaidie, Baba.

254 Sasa kulikuwa na mikono mingi, loo, dazeni moja au zaidi, iliyoinuliwa, labda zaidi. Kumi na mitano ama ishirini, waliotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo inathibitisha ya kwamba wana njaa, Bwana. Na Wewe umesema, "Heri wenye njaa." Kwa nini? Roho Mtakatifu tayari amezungumza nao. Nao wamebarikiwa, kuwa na njaa kwelikweli, wakijua ya kwamba Mungu yuko pamoja nao, na kuwapa hiyo njaa. Loo, wakijua ya kwamba kuna jambo fulani huko nje kwa ajili yao, maadamu tu wanalionea njaa! Kama tu vile mtu akiwa na njaa ya chakula, inabidi kuwe na chakula apate kula.

255 Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utamjaza kila mmoja wao. Jalia kwamba wajazwe na Roho Mtakatifu, hata kabla ya uamsho kuanza. Kabla mkutano huu haujakwisha usiku wa leo, jalia, Bwana, kwamba Roho Mtakatifu atamjia kila mwanadamu hapa na kujaza kila moyo kwa Nguvu na sifa Zake. Tujalie, Baba.

256 Sasa, waponye wagonjwa walio miongoni mwetu. Na, Mungu, uwe pamoja nasi, utubariki. Mbariki Ndugu yetu mpendwa Neville. Tunaomba ya kwamba utamdumisha mnyenyekevu, Bwana. Na umpe hayo mahubiri ya ajabu, yenye nguvu na mafundisho ambayo amekuwa akilitolea kanisa, tukijua ya kwamba ni Injili ile ile ya akili timamu, ya busara, isiyoghoshiwa ya Yesu Kristo. Mungu, mimina tu baraka juu yake. Mbariki mkewe na familia yake. Tubariki sote pamoja, wazee, kila mmoja, pamoja, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, Ndugu Teddy, hebu . . .

257 Una neno unalotaka kusema, Ndugu Neville, chochote kuhusu matangazo ya Jumamosi ijayo? Nadhani ni yote . . . [Ndugu Neville anasema, "Naam."—Mh.] Kwa ajili ya matangazo ya Jumamosi ijayo. Ni wangapi humsikiliza Ndugu Neville kwenye matangazo ya redio? Anayo, naamini, nusu saa sasa. Je, hiyo ni kweli? [Ndugu Neville anazungumza na Ndugu Branham.] Naam, endelea moja kwa moja.

[Ndugu Neville anasema, "Michango yoyote ya matangazo ya redio, usiku wa leo, mtu fulani anikabidhi tu hiyo baada ya ibada. Tutashukuru. Hatuna pesa za kutosha kabisa kwa matangazo ya Jumamosi, lakini itakuwa hapa wakati utakapowadia, kwa hiyo tunamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo. Mungu na awabariki sasa."—Mh.]

258 Ndugu Neville, simama pale pale mlangoni ambapo watu wanatokea, na ambapo, endapo wana kitu kwa ajili ya jambo hilo, ukipenda, ndugu. [Ndugu Neville anasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni sawa, kwa hiyo kama una uhakika kwamba umelipata sasa. Sasa, ni kwa ajili ya matangazo yake. Anajaribu kuweka hewani. Yeye hukutana na watu huko nje, pia watu ambao hawangekuja kwenye maskani hii.

Mara nyingi, nimefanya jaribio.

259 Watu wanasema, "Vema, Kasisi Branham, atakuja huku na kuniombea?"

Ninasema, "Njoo maskanini."

260 "Vema, uh, uh, unajua, uh, uh, siwezi kabisa kupata wakati wa kufanya hivyo."

261 Mnajua nini? Wana shingo ngumu sana, nusu ya wakati, kujinyenyekeza kuja kwenye hii. Hiyo ni kweli kabisa. Labda mchungaji wao anasema, kama mtu fulani akiwapata hapa, wanaogopa watakuwa katika kundi baya. Endapo wanawazia hayo, haingefaa chochote kuwaombea, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli.

262 Mnajua yale nabii aliyomwambia Naamani? Alisema, "Shuka ukajichovye katika Yordani, maji yake yaliyojaa matope na ni machafu."

263 Akasema, "Mbona, maji katika nchi yangu ni safi kuliko hayo."

264 "Vema, rudi pamoja na ukoma wako basi" hiyo ni kweli, mpaka alipojinyenyekeza na kwenda kule kwenye mto Yordani uliojaa matope, na kujizamisha mara saba kama vile nabii alivyomwambia. Ukoma wake ukamwacha. Hiyo ni kweli.

265 Ikiwa wao ni wagumu na baridi sana hata hawawezi kuja maskanini, basi wao . . . wanaweza kubaki na ukoma wao basi. Hiyo ni kweli kabisa. Mungu, uturehemu!

266 Loo, jamani, marafiki, ninapoona ile siku ikija, nikiona umri wangu ukipenya hapa, na kila kitu, nimefanya nini? Loo, najisikia kana kwamba sijafanya chochote. Sina budi kumfanyia kitu Bwana Yesu. Si—sina budi kweli kufanya kitu. Loo, mimi. . .moyo wangu unanitoka sasa. Najisikia vizuri na mwenye nguvu. Wala si—sijui la kusema. Sijawa nikihubiri kwa miaka mingi, nami ninaondoka sasa kuanza kuhubiri. Kabisa sijui la kufanya, lakini ninataka kuwaleta watu kwa Kristo. Hiyo ni. . .Nataka kumfanya mtu awe sawa na Mungu. Ni hayo tu. Na hata hivyo, mle ndani, najisikia kama vile i—ile huduma aliyonipa, na hata hivyo nimemletea zaidi ya watu nusu milioni. Lakini, hiyo, hiyo inaonekana ndogo sana, kwa mabilioni walioko ulimwenguni, wasio Wakristo, mnaona.

267 Waangalieni tu hao mamilioni na mamilioni na mamilioni ambao hawajaendewa bado! Hima twendeni, marafiki. Hima twendeni. Labda huwezi kuvuka bahari, lakini unaweza kuvuka barabara. Hebu tufanye jambo. Hebu tufanye jambo kwa utukufu wa Mungu.

Mungu awabariki, tunaposimama sasa.

268 Ninataka kuwaulizeni sasa, tunapoimba wimbo wetu wa kufumukana, *Peleka Jina La Yesu*. Angalieni, peleka Jina la Yesu, kama ngao dhidi ya kila adui. Hiyo ni kweli. Majaribio yanapokuzunguka, taja Jina Lake takatifu katika maombi. Ni wangapi watakaolipeleka, usiku wa leo, wakisema, "Mungu, nitakupenda, Bwana Yesu. Ninataka uende pamoja nami?" Inueni mikono yenu juu sana sasa. Hiyo ni sawa. Mungu awe pamoja nanyi, ndugu na dada yangu Mkristo. Sawa.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na wa majonzi;
Li—litakupa furaha na faraja,
Lipeleke kila uendako.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha. . .

269 Sasa tunapoimba aya ya pili, geuka na kupeana mikono na mtu aliye karibu nawe sasa.

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo ni tamu jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;

Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo ni
tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na . . .

270 Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Je, mnanipenda? Semeni . . . [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nataka mfanye jambo fulani. Kuna tofauti kidogo hapa kote maskanini. Tunataka kuwa kundi kubwa la kirafiki, mnaona. Hebu tupeane mikono na kila mtu. Usisimame kwa mtu mmoja kwa muda mrefu sana. Nyosha tu mkono umpe mwingine, "Nina furaha kuwa nawe, ndugu. Karibu tena. Nina furaha kuwa nawe, dada. Mungu akubariki." Peana mikono na kila mtu. Mkitaka kutembeleana, mwaweza kwenda nyumbani mkatembeleana. Lakini hebu tupeane mikono na kila mtu. Mnaona? Zungukeni mkapeane mikono na kila mtu, kisha mtoke nje ya jengo, mkishangilia. Si mtafanya hivyo? Mungu awabariki.

271 Tunapoinamisha vichwa vyetu. Ndugu Ruddell, kule nyuma, utaturuhusu tufumukane kwa maombi tafadhali, Ndugu Ruddell.

54-1024 Dhambi Isiyosameheka
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org